SUPA JACKPOT
TZS. 1,029,401,974
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



UKURASA 2

## DC ashtuka watoto kunajisiwa wakiwa kwenye magari ya shule


BUFE
Nipashe
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA
Ulivyo uvamizi wa tembo shambani ukisambaratisha mkulima kijijini

UKURASA 11

# Nipashe

Ijumaa Septemba 9, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581063

www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

## MTUMISHI KUTOKA SUMBAWANGA APEWA CHEO KINACHOOGOPWA

UKURASA 8

## SAKATA LA TOZO

# CCM yataka hatua kunusuru wananchi



Katibu wa Halmashauri Kuu ya Taifa ya CCM, Itikadi na Uenezi, Shaka Hamdu Shaka, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**



UKURASA 2

Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba

## Majaliwa ang'aka kibanda cha mlinzi kugharimu mil. 11/-

UKURASA 8

UKURASA WA 3

### KOREA YAIPATIA TANZANIA MKOPO TRIL. 2.3/- MIRADI YA MAENDELEO

SERIKALI ya Jamhuri ya Korea Kusini imeipatia Tanzania mkopo nafuu wa Dola za Marekani bilioni moja (Sh. trilioni 2.3)...

UKURASA WA 4

### SAMIA ATAKA MAFUNZO YA UONGOZI YAPELEKWE NGAZI YA WILAYA, MIKOA

RAIS Samia Suluhu Hassan, amekitaka Chuo cha Taifa cha Ulinzi (NDC), kupeleka mafunzo ya uongozi yanayotolewa kwa viongozi wakuu kwenye ngazi ya mikoa na wilaya. Alitoa kauli hiyo jana wakati wa kilele cha maadhimisho ya miaka 10 ya chuo hicho...

UKURASA WA 4

### TAASISI YA MO DEWJI YATOA MILIONI 100/- MUHIMBILI



TAASISI ya Mo Dewji imetoa msaada wa Sh. milioni 100 ili kusaidia matibabu ya watoto wanaougua saratani...

## Mbaroni tuhuma za kuwatapeli wanawake

UKURASA 3

**MICHEZO** MGUNDA AFUNGUKA SIMBA ITAPAMBANA UK.24

**KABWELA** UK. 18

# DC ashtuka watoto kunajisiwa wakiwa katika magari ya shule

**Na Elizabeth Zaya**

MKUU wa Wilaya la Kinondoni, Godwin Gondwe, amesema wilaya hiyo inatarajia kutunga sheria ndogo ili kuwataka wamiliki wote wa shule za msingi na sekondari kuajiri matroni wa magari ya shule ili asimamie wanaposafirishwa kwenda shuleni na kuwarudisha nyumbani.

Hatua hiyo inalenga kukabiliana na vitendo vya kikatili ambavyo watoto wamekuwa wakifanyiwa wanapokuwa kwenye magari hayo, ukiwamo unajisi.

Gondwe alitoa kauli hiyo jana alipowasilisha salamu za wilaya katika Mkutano wa Wadau wa Ustawi wa Jamii nchini uliofanyika mkoani Dar es Salaam.

Alisema wamepanga kuchukua hatua hiyo kutokana na kuendelea kuripotiwa matukio mengi ya watoto kufanyiwa ukatili wakiwa kwenye mabasi wakati wakienda shuleni na wanaporudishwa nyumbani.

"Kutokana na matukio mengi kuripotiwa ya watoto kufanyiwa ukatili wakiwa kwenye mabasi ya shule wakati wa kwenda shuleni na kurudi nyumbani, tumeamua kutunga na kupitisha sheria ndogo ambayo itamtaka kila mmiliki wa shule aajiri matroni ambaye atakuwa muambata kwenye magari yote ya shule kwenye wilaya yetu, hii ni katika kuwalinda watoto dhidi ya ukatili huo," alifafanua.

"Tumekuwa tukipokea matukio mengi ya watoto kufanyiwa ukatili kwenye mabasi ya shule na juzi kuna mama mmoja alikuja ofisini kwangu kuripoti tukio la namna hiyo.

"Bahati nzuri mtoto kutokana na urafiki wake na mama yake alieleza jinsi alivyonusurika kufanyiwa ukatili huo baada ya kupiga kelele," alisema.

Gondwe alisema kuwa mbali na jitihada hizo wanazochukua, pia kwa sasa wameongeza nguvu ya kukabiliana na vitendo vya ukatili kwenye eneo la fukwe za Coco baada ya kuwapo kwa kisa cha mtu mmoja anayetoa huduma eneo hilo kudaiwa kumbaka binti aliyekuwa akimfundisha kuogelea.

Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Amoni Mpanju, alisema serikali iko mbioni kukamilisha mwongozo utakaowataka watu wote wenye taasisi kuhakikisha wanaajiri maofisa ustawi wa jamii kwenye taasisi zao.

"Kuna haja ya kuanza kutoa huduma za ustawi wa jamii, sisi wizara tunakuja na mkakati tofauti kuhakikisha kila mwajiri atakayesajili shule na taasisi kubwa, ni lazima kuwa na watu wa ustawi wa jamii," alisema Mpanju.

Mnamo Februari 2020, Nipashe ilichapisha ripoti maalum iliyoangazia kwa kina madhila yanayowakumba wanafunzi, hasa wenye umri mdogo, wakilawitiwa wakiwa shuleni na nje kidogo ya mazingira ya shule wilayani Mkuranga mkoani Pwani.

Katika uchunguzi wake, Nipashe ilibaini vitendo hivyo vinafanywa dhidi ya watoto na ama ndugu zao, vijana wa mitaani ama wanafunzi wenzao wa madarasa ya juu.

Nipashe ilipofika wizarani, kipindi hicho Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, ilipata ufafanuzi wenye takwimu kwamba mikoa hatari zaidi kwa vitendo hivyo ni Dar es Salaam, Tanga na Pwani.



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi (kushoto), akimwapisha Ali Abdalla Ali, kuwa Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar (ZAECA), Ikulu jijini Zanzibar jana. **PICHA: IKULU**

# CCM yataka hatua sakata la tozo

**Na Beatrice Shayo**

KAMATI Kuu ya Halmashauri Kuu ya Taifa (CC-NEC) ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), imeielekeza serikali kutazama na kuchukua hatua kuhusu tozo za miamala ya kielektroniki iliyoanza kutekelezwa hivi karibuni.

Katika kuchukua hatua hizo, chombo hicho nyeti cha CCM kimeitaka serikali kuzingatia ushauri na maoni ya wananchi.

Katibu wa NEC Itikadi na Uenezi wa CCM, Shaka Hamdu Shaka, alisema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu yaliyojiri kwenye kikao cha CC-NEC kilichofanyika juzi chini ya Mwenyekiti wa CCM Taifa, Rais Samia Suluhu Hassan.

"Baada ya kutafakari na kujadiliana kwa kina, Kamati Kuu imeona umuhimu wa serikali kusikiliza maoni na ushauri wa wananchi kuhusu utekelezaji wa bajeti, hususani katika eneo la tozo za miamala ya kielektroniki iliyoanza kutekelezwa hivi karibuni," alisema Shaka.

Alisema Kamati Kuu ilipokea, kutafakari na kujadili kwa kina kuhusu hatua za kibajeti zinazoendelea kuchukuliwa kwa lengo la kupata fedha za kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo kwa kasi ili kuwawekea wananchi mazingira mazuri ya kujipatia maendeleo na utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020-2025.

"Eneo mojawapo ni tozo. Ni ukweli usiopingika kwamba serikali imefanya mambo makubwa katika kipindi kifupi mfano ujenzi wa vituo vya afya 234 na shule mpya za sekondari 214 na maeneo mengine kadhaa ambayo yanagusa maisha ya kila siku ya Watanzania.

Baada ya kutafakari na kujadiliana kwa kina, Kamati Kuu imeona umuhimu wa serikali kusikiliza maoni na ushauri wa wananchi kuhusu utekelezaji wa bajeti hiyo hususani katika eneo la tozo za miamala ya kielektroniki,' alisema.

Shaka alisema maelekezo hayo yamezingatia ibara ya 20 (b) ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020 inayoeleza kuongeza upatikanaji wa huduma za kifedha kwa gharama nafuu kwa kupanua wigo wa matumizi ya TEHAMA katika utoaji wa huduma za kifedha ili kuongeza huduma jumuishi za fedha nchini, kuchochea uwekezaji wa ndani na kukidhi mahitaji halisi ya wananchi hususani wa kipato cha chini na waishio vijijini.

Shaka alisema Kamati Kuu ya CCM imeielekeza serikali kufikiria na kujielekeza katika kubana matumizi serikali, kuendelea kujenga mazingira rafiki na wezeshi ili kujenga uchumi imara unaozalisha kwa lengo la kutanua wigo wa kodi na kubuni vyanzo vipya ya kodi ili kuwa na viwango vya pamoja na mfumo rafiki wa kodi kwa kila mmoja.

Kiongozi huyo alisema Watanzania wanapaswa kumpongeza Rais Samia kwa namna alivyoimarisha uhuru wa habari, kujieleza na kuheshimu misingi ya utawala bora.

Alisema nchi ina Rais ambaye anashaurika na yuko tayari kusikiliza vilio na macho yake yapo kwa wananchi wake kwa kufuatilia mwenendo mzima yanayoendelea Tanzania na ametoa uhuru kwa kila Mtanzania.

Shaka alisema katika jambo hilo, chama kimesikiliza kwa sababu wao ndio wenye serikali na maelekezo hayo yamo katika Ilani ya Uchaguzi Ibara ya 303 inavyoelekeza kusikiliza kero za wananchi, inayoeleza:

"Ili CCM iendelee kukubalika na kuaminiwa na wananchi na kupewa ridhaa ya kuongeza nchi, uko umuhimu mkubwa kwa viongozi wa CCM kuwa karibu na wananchi kwa kuwatembelea, kusikiliza kero zao na kushirikiana nao katika kuzipatia majawabu.

Ni muhimu kwa CCM wakati wote kuwa kimbilio la wasemaji na watetezi hasa wanyonge."

Kutokana na hali hiyo, alisema CCM imetimiza wajibu wa msingi wa kusikiliza maoni ya wananchi wa Watanzania na kuamua kuishauri serikali, hivyo chama kitafuatilia kwa umakini vikwazo, hivyo wananchi wawe watulivu suala hilo la tozo litashughulikiwa.

"Kila kwenye vikwazo Chama Cha Mapinduzi kitahakikisha kinapunguza vikwazo hivyo kwa ushirikishwaji wa moja kwa moja kwa kila Mtanzania," alisema.

Shaka alisema yale yote waliyokubaliana katika Kamati Kuu yatashughulikiwa muda si mrefu, hivyo Watanzania waendelee kumwamini Rais Samia kwa kuwa ana nia njema ya kuwasaidia wananchi kuondokana na changamoto mbalimbali.

# Korea yaipatia Tanzania mkopo tril. 2.3/- miradi ya maendeleo

**Na Gwamaka Alipipi**

SERIKALI ya Jamhuri ya Korea Kusini imeipatia Tanzania mkopo nafuu wa Dola za Marekani bilioni moja (Sh. trilioni 2.3), kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2021 hadi 2025.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana baada ya utiaji saini wa mkataba huo, Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango, Emmanuel Tutuba, alisema sehemu ya fedha hizo, Sh. bilioni 163.1 zitatumika kutekeleza mradi wa upanuzi wa mfumo wa vitambulisho vya taifa awamu ya pili.

Tutuba alisema Sh. bilioni 151. 5 zitatumika kutekeleza mradi wa uboreshaji wa miundombinu ya taifa ya taarifa za ardhi.

Alisema pia zinakwenda kutekeleza mradi wa uendelezaji wa mifumo ya usambazaji wa majisafi na ya kutibu majitaka, kwa kutengewa Sh. bilioni 163.1.

Kadhalika, Tutuba alisema Sh. bilioni 186.4 zinakwenda kutekeleza mradi wa ujenzi wa Chuo cha Kisasa cha Mafunzo ya Usafirishaji wa Reli.

"Orodha ya miradi iliyoibuliwa inahusisha miradi mingine ambayo ni pamoja na Ujenzi wa Hospitali ya Binguni, Zanzibar kwa Dola za Marekani milioni 100 (Sh. bilioni 233) na mingine katika sekta ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano, afya, nishati na miundombinu".

Tutuba alisema hayo ni makubaliano ya awamu ya nne kati ya Tanzania na Jamhuri ya Korea Kusini tangu kuanzishwa kwa Mfuko wa Ushirikiano wa Kiuchumi na Maendeleo wa Korea (EDCF) hapa nchini mwaka 2004.

Alisema makubaliano ya awamu ya kwanza yalikuwa na Dola za Marekani milioni 140 yakihusisha kipindi cha kuanzia mwaka 2011 hadi 2013, makubaliano ya awamu ya pili yalikuwa na Dola za Marekani milioni 200 yakihusisha kipindi cha kuanzia mwaka 2015 hadi mwaka 2018.

Tutuba alisema makubaliano ya awamu ya tatu yalikuwa na Dola za Marekani milioni 300 yakihusisha kipindi cha kuanzia mwaka 2018 hadi mwaka 2020.

"Fedha zilizotokana na makubaliano haya, zilitumika kufadhili miradi mbalimbali katika sekta za miundombinu ya usafirishaji, elimu, afya, nishati na maji.

"Mifano mizuri ni, mradi wa ujenzi wa Daraja jipya la Selander linalojulikana kama Tanzanite ambalo siyo tu kwamba limebadilisha sura ya Dar es Salaam, lakini limepunguza msongamano wa magari katika Barabara ya Ali Hassan Mwinyi na mradi wa ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji Zanzibar."

Balozi wa Jamhuri ya Korea hapa nchini, Kim Sun Pyo, alisema kuingiwa kwa mkataba huo ni matunda ya ushirikiano wa nchi hizo na kwamba wataendelea kutoa fedha ili kufadhili miradi mingine.



Ofisa Mtendaji wa Masoko wa East Africa Radio/Television, Carine Maro (kushoto) na Meneja Mradi wa The Work Ltd, Ahmed Ally, wakitiliana saini makubaliano jijini Dar es Salaam jana ya ushirikiano wa miaka miwili utakaohusisha usimamizi wa matamasha mbalimbali ya burudani. **Habari zaidi Uk. 23. PICHA: MIRAJI MSALA**

# Mbaroni tuhuma za kuwatapeli wanawake

**Na Idda Mushi,** MOROGORO

JESHI la Polisi mkoani Morogoro limewanasa watu wawili wakazi wa Kihonda Manyuki mjini Morogoro na Buza, Dar es Salaam kwa tuhuma za kuwarubuni wanawake wenye kipato na kuwawekea dawa za kulevya kwenye vinywaji au supu.

Baada ya kuwafanyia hivyo, watu hao huwaibia fedha simu na mali zingine na baadhi yao kuwaingilia kimwili bila ridhaa yao.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Fortunatus Musilimu, alikiri jana kukamatwa kwa watu hao kwa nyakati tofauti kwa madai ya kujihushisha na vitendo hivyo kwenye mikoa mbalimbali nchini ikiwamo Morogoro, Dodoma, Mwanza na Dar es Salaam.

Aliwataja watuhumiwa hao kuwa ni Paulo Shayo (48) mkazi wa Kihonda Maduka 10, Manispaa ya Morogoro na Dixon Mwashambo (33) maarufu kama Tajiri Maswe au Papaa, mkazi wa Buza Tanesco, Dar es Salaam ambaye hujihusisha na shughuli za udalali.

Kamanda Musilimu alisema watu hao kwa nyakati tofauti wamekuwa wakitumia unadhifu wao, magari ya kifahari na ya gharama kubwa, kuwarubuni kimapenzi na kujenga uhusiano na wanawake hasa wenye kipato kikubwa na kuwapeleka kwenye hoteli kubwa, wakiagiza vyakula na vinywaji vya gharama kubwa.

Pia alisema watuhumiwa hao huwawekea wanawake hao dawa za kulevya zinazosadikiwa kuwa ni vidonge vinavyoyeyuka kirahisi kwenye supu au vinywaji na hatimaye wanapoanza kuvurugikiwa hutoa namba za siri za benki, simu na taarifa zingine nyeti kisha kuwaibia.

Kuhusu Shayo, alisema amekuwa akitumia mbinu ya kuwapeleka wanawake kwenye hoteli za kifahari na kuwapa vitambaa vya kufutia jasho (leso) viinavyosadikiwa kuwa na dawa za kulevya, hivyo muda mfupi baada ya kuvitumia kupoteza fahamu kisha kutekeleza uhalifu.

Musilimu alibainisha moja ya matukio ya hivi karibuni alilofanya ni kwenye hoteli ya Cate iliyoko barabara kuu ya Morogoro- Dar es Salaam mjini Morogoro, eneo la Kingoluwira.

Alisema mtuhumiwa huyo alimwibia binti mwenye umri wa miaka 30 mkazi wa Dakawa na mdogo wake mwenye umri wa miaka 28 mkazi wa Kihonda Bima, fedha tasilimu Sh. milioni 1.6 na simu mbili aina ya Vivo na iPhone 7.

Papa au Tajiri Maswe, Musilimu alisema amekuwa akitumia mbinu ya kuvaa kwa unadhifu na kujifanya ni mtumishi wa Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) makao makuu, Dodoma.

Katika kutekeleza uhalifu wake, alisema mtu huyo akikutana na mwanamke ambaye ameshamrubuni hununua supu au mvinyo mwekundu (red wine) na kuweka dawa za kupoteza kumbukumbu kisha kumfanya atoe namba za siri za kampuni za simu na akauti za benki na kuwa rahisi kumwibia.

"Tukio la karibuni, mtuhumiwa Mwashambo alilifanya baada ya kuingia Morogoro majira ya saa 12:00 jioni akitokea Dar es Salaam. Alimwibia binti mwenye umri wa miaka 27, mkazi wa Mlandizi mkoani Pwani kwa kuchukua Sh. milioni 7.45, simu aina ya iphone 8+ na saa aina ya Rado," alisema Musilimu.

Alisema mtuhumiwa alimrubuni mwanamke huyo baada ya kumwomba msaada wa usafiri baada ya basi kuharibika njiani eneo la Dumila, badala yake akampeleka binti huyo hadi kwenye kwenye nyumba ya kulala wageni ya SAS iliyoko mjini Morogoro.

Kwa mujibu wa Kamanda Musilimu, mtuhumiwa huyo anadaiwa amekuwa akibaka na kuwalawiti watu anaofanikiwa kuwarubuni na amekuwa alijihusisha na matukio hayo ya kiuhalifu katika mikoa ya Dar es Salaam, Arusha na Mwanza.


## TAARIFA KWA UMMA

Tanzania Mobile Network Operators Association (TAMNOA)

**DAR ES SALAAM, SEPTEMBA 8, 2022.**

Kutokana na tozo za miamala ya simu zilizoanza mwaka 2021 mwezi Julai, na tukiangalia mlolongo wa matukio tangu kuanzishwa kwa tozo hizi, pamoja na kupungua kwa matumizi ya huduma za kifedha hali ya mwaka huu wa fedha ni ya kuridhisha.

Hali hii ya kuridhisha imetokana na mazungumzo ya kina baina ya watoa huduma, wadau na serikali tangu tozo hizo zilizolenga kuongeza kasi ya ufikishwaji wa huduma kwa jamii, zilipoanza mwaka jana. Maongezi hayo yalipelekea punguzo la hadi asilimia 60% hadi sasa ambapo asilimia 30% ilipunguzwa kufikia asilimia 70% mnamo mwezi wa tisa mwaka jana mara tu baada ya tozo hizo kuanza ambapo mwenendo wa kurudi wigoni kwa wateja ulianza kuonekana. Hadi kufikia mwaka huu wa fedha wa serikali 2022, asilimia 43% nyingine ilipunguzwa kutoka kwenye asilimia 70% iliyosalia sawa na asilimia 30% kutoka mwanzoni hali ambayo imeendelea kudhihirisha uwepo wa mandhari shirikishi kati ya watoa huduma na serikali pale changamoto zinapojitokeza.

Kwa sasa muonekano wa kibiashara unaendelea kuwa wenye hali nzuri na tunategemea kuendelea kushirikiana na serikali kukuza sekta na kufikisha huduma zake jumuishi kwa watanzania wote.

217038102

# Samia ataka mafunzo ya uongozi yapelekwe ngazi ya wilaya, mikoa

**Na Elizabeth Zaya**

RAIS Samia Suluhu Hassan, amekitaka Chuo cha Taifa cha Ulinzi (NDC), kupeleka mafunzo ya uongozi yanayotolewa kwa viongozi wakuu kwenye ngazi ya mikoa na wilaya.

Alitoa kauli hiyo jana wakati wa kilele cha maadhimisho ya miaka 10 ya chuo hicho yaliyofanyika mkoani Dar es Salaam, huku akitaka jambo hilo lifanyiwe kazi kwa uharaka.

"Pamoja na mafanikio tunayosherehekea leo, kuna masuala ambayo ningependa kuona yanatimia muda mrefu na mfupi ujao.

Aliongeza: "Mojawapo ni kwenda kufundisha mafunzo haya ngazi za chini, wilaya na mikoa ambazo zinaishi na watu, sasa imefika wakati chuo kijielekeze kutoa kozi huko chini na kama kutahitajika msaada serikali tuko tayari kushirikiana nanyi. Tunataka nchi iwe na wazalendo wa kweli ambao wanaitumikia nchi."

Rais Samia alisema kwa sasa serikali inajielekeza zaidi kukuza uchumi wa wananchi ikiwamo kuleta mapinduzi ya kilimo na kuwa ni lazima huko chini kwenye wilaya na mkoa wawe na upeo wa kuitumikia nchi yao.

Aidha, alikipongeza chuo hicho kwa kuwafundisha viongozi mbinu za umahiri za uwezo wa kuona mbali.

"Kufundisha mbinu za kuhitimu na uwezo wa kuona mbali kama alivyosema mkuu wa chuo ni jambo muhimu sana kwa sababu dunia ya leo haiko tulivu, inabadilika kila uchwao, kwa hiyo ni lazima tuwe na watu wanaoisoma kila inapokwenda, wanasoma huko kutatokea nini na watabiri," alisema Rais Samia.


"Kwa sasa tunafungua nchi na unapofungua, wageni ni wengi wawekezaji ni wengi, kwa hiyo ni lazina kuwe na watu ambao wanasoma mipango ya kujenga nchi kule mbele tunakokwenda.

"Niombe sana kutanua wigo wa watu wanaoingia hapa, pia kama mlikuwa mnaenda na kozi tatu, nne, ziongezeke. Watalii wameingia sana lakini nani anaangalia kwamba huyu ni mtalii au anaingia kivingine, nani anaangalia? Kufunguka kwetu kwa nchi kusihatarishe usalama wetu."

Alikitaka chuo hicho kutekeleza sera ya serikali ya upatanishi.

Kadhalika Rais Samia alitoa wito kwa wizara na taasisi kuteua watu wenye sifa hususani vijana ikiwa ni pamoja na kutoa kipaumbele kwa wanawake wanaofanya vizuri katika chuo hicho.

Alisema serikali ipo tayari kutoa ushirikiano kwa chuo hicho katika ujenzi wa chuo cha kivita kama ambavyo kimeomba.




Janeth Mashauri na Frank Kinabo (wa pili kushoto), kutoka Taasisi ya Mo Dewji, wakikabidhi mfano wa hundi ya Sh. milioni 100 kwa Mwenyekiti wa Bodi ya Taasisi ya Tumaini la Maisha (TLM), Dk. Gerald Mongella, jijini Dar es Salaam jana, ikiwa ni mwendelezo wa ushirikiano baina ya Taasisi ya Mo Dewji na Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH) kupitia TLM. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Taasisi ya Mo Dewji yatoa milioni 100/- Muhimbili matibabu saratani

**Na Mwandishi Wetu**

TAASISI ya Mo Dewji imetoa msaada wa Sh. milioni 100 ili kusaidia matibabu ya watoto wanaougua saratani katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH).

Fedha hizo zilikabidhiwa jana jijini Dar es Salaam kwa Tumaini La Maisha (TLM), asasi ambayo inajishughulisha na matibabu ya watoto wanaougua saratani.

Katika makabidhiano hayo, uongozi wa Taasisi ya Mo Dewji ulibainisha kuwa tangu mwaka 2013, umekuwa unashirikiana na Hospitali ya Taifa ya Muhimbili kupitia TLM, ambacho ni kituo kikubwa zaidi cha saratani ya watoto Afrika Mashariki.

Taasisi hiyo inaangazia elimu, maendeleo ya jamii, afya na uwezeshaji wa kijinsia, ikiamini kuwa huduma bora za afya zinazopatikana ni haki kwa binadamu na inajitolea kuboresha huduma za afya kote nchini.

Wawakilishi wa taasisi hiyo walibainisha jana kuwa wanaendelea kufanya kazi na TLM kwa kuwa programu zao ni muhimu kwa maisha ya maelfu ya wakazi wa Afrika Mashariki.

Walisema programu zao hutoa huduma za kiafya na zisizo za kiafya kwa watoto, kama vile ununuzi wa dawa za Kemotherapy, usaidizi kwa programu ya shule, matengenezo ya mpango wa usafiri kwa wagonjwa na walezi wao, usaidizi wa programu ya tiba ya michezo kwa wagonjwa, usaidizi katika mafunzo ya stadi za maisha kwa wazazi, vifurushi kwa wagonjwa wapya waliolazwa na usaidizi wa mshahara kwa wafanyikazi ambao siyo wa afya.

Uongozi wa taasisi hiyo pia uliwahimiza watanzania wote kuunga mkono juhudi za TLM na mashirika mengine yasiyo ya kiserikali yanayojishughulisha na kuwawezesha watu wengi wasiojiweza nchini.

Mbali na msaada huo wa fedha, taasisi hiyo pia ilikabidhi vifaa mbalimbali kwa ajili ya matumizi ya kila siku ya watoto hao.

Machi mwaka huu, serikali kupitia Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, iliipongeza Taasisi ya Mo Dewji kwa kujitoa na kuchangia mambo makubwa kwenye sekta ya afya.

Waziri Ummy pia aliiomba taasisi hiyo kusaidia jitihada za serikali kukabiliana na uhaba wa madaktari bingwa wa mishipa ya fahamu, akibainisha kuwa Tanzania ina uhaba mkubwa kwenye eneo hilo.

Ummy alitoa pongezi hizo jijini Dar es Salaam wakati wa sherehe ya kutimiza kwa miaka minane ya Taasisi ya Mo Dewji Foundation.

Alisema serikali inatambua mchango na juhudi zinazofanywa na taasisi hiyo katika sekta mbalimbali ikiwamo afya, akisifu kujitolea kwake pale inapobaini kuna upungufu.

"Taasisi ya Mo Dewji imegharamia watoto 100 wenye tatizo la saratani ya damu kupitia Mfuko wa Tumaini la Mama, lakini pia ametusaidia vifaa tiba kwa ajili ya watoto njiti.

"Hapa niseme tu kwa nchi zilizoendelea, kuzaliwa kabla ya muda siyo tatizo. Kwa hiyo, hivyo vifaa vilivyotolewa na Taasisi ya Mo Dewji vimetusaidia katika kuokoa watoto wachanga," alisifu.

Mwanzilishi wa Taasisi ya Mo Dewji, Bilionea Mo Dewji, alimshukuru Waziri Ummy kuhudhuria sherehe hiyo na kumwahidi kushirikiana naye zaidi katika sekta ya afya ikiwamo kufadhili masomo ya madakatari bingwa wa ubongo na mishipa ya fahamu aliloombwa na serikali.

Mo Dewji alisema alianzisha taasisi hiyo mwaka 2015, akiwa na ndoto ya kuboresha maisha ya jamii ya kitanzania, akilenga sekta za afya, maendeleo ya jamii na elimu ili kukabiliana na umaskini nchini.

# Maambukizi corona yaendelea kupungua

**Na Romana Mallya**

WAZIRI wa Afya, Ummy Mwalimu, amesema maambukizi ya ugonjwa wa UVIKO-19 (corona) yanaendelea kupungua, ikiwamo makali yaliyokuwa yakisababisha watu kulazwa, uhitaji wa hewa ya oksijeni, mashine za kusaidia kupumua na vifo.

Amesema mafanikio hayo yametokana na mwitikio wa wananchi kupata chanjo ya ugonjwa huo.

Ummy alitoa taarifa hiyo jana mkoani Dar es Salaam wakati akieleza mwenendo wa ugonjwa wa Uviko-19.

Alisema tangu kutangazwa kwa ugonjwa huo nchini Machi, mwaka 2020 mpaka Septemba 7, mwaka huu, visa 35,747 vilithibitishwa kuwa na maambukizi ya UVIKO-19 na vifo vilivyotokea ni 808.

"Uchambuzi wa takwimu katika Maabara ya Taifa ya Afya ya Jamii na vituo vya kutolea huduma za afya kwa Septemba 7, mwaka huu, unaonyesha kuwa kati ya watu 289 waliopimwa watu 23 wamethibitika kuwa na maambukizi ya ugonjwa wa UVIKO-19.

Alisema kati ya wagonjwa hao waliolazwa saba hawajapata chanjo ya UVIKO-19 na kati yao, mgonjwa mmoja alikuwa anatumia oksijeni. Takwimu hizi zinathibitisha ugonjwa huu bado upo," alisema.

Waziri Ummy alisema maambukizi mapya yameonekana kupungua yakichangiwa na upataji wa chanjo, kwamba asilimia 60 ya walengwa wenye umri wa miaka 18 wamechanjwa.

Alisema Shirika la Afya Duniani (WHO) linasisitiza kuwa hatari ya ugonjwa huo bado ipo na kushauri afua za kinga ziendelee kuzingatiwa kwa kutathimini masuala mbalimbali ikiwamo hali ya maambukizi, kiwango cha kupata chanjo, uwezo wa upimaji na mifumo ya afya nchi husika kuhimili idadi kubwa ya wagonjwa.

Alisema kutokana na mwenendo wa ugonjwa huo, serikali inaendelea kuelimisha wananchi kuhusu kupata chanjo, kufanya uchunguzi wa afya dhidi ya magonjwa ya milipuko kwa wasafiri wa kimataifa katika viwanja vya ndege vya kimataifa na kusisitiza kufanya vipimo vya haraka kwa wasafiri wanaoingia nchini.

Waziri Ummy alisema kwa sababu ugonjwa huo bado upo, wanawasisitizia wananchi kuendelea kufuata taratibu za unawaji wa mikono kwa maji tiririka, sabuni au vitakasa mikono na wale wenye umri wa miaka 18 na kuendelea kuhakikisha wanapata chanjo.

Kadhalika, waziri huyo aliwahimiza wazee, watu wenye magonjwa sugu na ambao hawajapata chanjo kamili wajitokeze kuchanja.

# Matapeli dhahabu bandia wavamia Sengerema

**Elizabert Seleman,**
SENGEREMA

WIMBI la matapeli wanaouza dhahabu bandia limeibuka na kuwatapeli fedha baadhi ya wananchi katika wilaya ya Sengerema mkoani Mwanza.

Wakizungumzia matukio hayo ya kutapeli, baadhi ya wananchi wilayani hapa walisema kitendo hicho kinachofanywa na matapeli hao hakivumiliki katika jamii kwa kuwa kinarudisha nyuma maendeleo ya wananchi na kuiomba serikali kuingilia kati suala hilo.

Wananchi hao walisema matapeli hao wanawapa kitu ambacho ni kigumu na kimefungashwa kwenye chuma na kinakuwa kimepakwa rangi mfano wa dhahabu na wanaambiwa wasikifungue mpaka wafike sehemu ya kuuzia.

Walisema matapeli hao wamekuwa wakitoka sehemu ambayo haijulikani na kujifanya kama wanauza dhahabu jirani na kituo cha mafuta cha Tabasam.

Kwa upande wake mmiliki wa kituo cha Tabasam ambaye ni Mbunge wa Sengerema, Hamisi Tabasam, alikiri kupokea malalamiko ya wananchi wake.

Alisema wananchi hao wamekuwa wakitapeliwa fedha kwa kununua dhahabu bandia na kuwatahadharisha kuwa makini dhidi ya matapeli hao.

Mbunge huyo tayari alisema amewasiliana na mkuu wa operesheni maalumu katika kituo cha polisi wilayani Sengerema ili kuwasaka matapeli hao na kuwachukulia hatua za kisheria.



Askari wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, akijaribu kuzima moto ulioteketeza nyumba ya Ester Mbasa, mkazi wa Majengo Mapya, Manispaa ya Shinyanga jana. Hakuna mtu aliyedhurika katika tukio hilo. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Mkurugenzi mpya ZAECA aahidi kuwashughulikia wezi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MKURUGENZI Mpya wa Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar (ZAECA), Ali Abdallah Ali, amesema kuwa atahakikisha anatenda haki na uadilifu kuchukua hatua kwa wote waliohusika na wizi wa fedha waliobainishwa katika Ripoti ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG).

Aliyasema hayo jana Ikulu mjini hapa wakati akizungumza na waandishi wa habari, baada ya hafla ya kula kiapo mbele ya Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, kuitumikia nafasi hiyo.

Uteuzi wake unatokana na aliyekuwa mtangulizi wake kujiuzulu nafasi hiyo baada ya Rais Mwinyi kutoridhika na utendaji wa ZAECA.

Alisema atahakikisha fedha za umma, matumizi ya umma na mali za umma zinatumika vizuri kwa maslahi ya wananchi wote wa Zanzibar.

"Yale ambayo mheshimiwa Rais ameyaagiza ni wakati wangu sasa kwenda kuyashughulikia kwa nguvu zote, kuhakikisha kwamba nayafanyia kazi na zaidi kuchukua hatua katika kuzingatia misingi ya haki na uadilifu na kwa kuanza nitaanzia katika ripoti ya CAG na kuangalia maeneo mengine ambayo yanaonesha ubadhirifu," alisema.

Rais amemuagiza kuanza kuifanyia kazi ripoti ya CAG na ubadhirifu wa umma upo katika maeneo mengi hivyo kulishughulikia hilo na kuchukua hatua kwa watakaohusika na ubadhirifu.

Rais Mwinyi alimpa maelekezo Mkurugenzi huyo mpya, kuifanyia kazi ripoti ya CAG na angependa kuona katika maeneo yote yaliyotajwa kuwa na kasoro uchunguzi wa kina unafanyika na hatua stahiki zinachukuliwa.

Alitaka ZAECA kutimiza wajibu wake na kumkumbusha sio vizuri kupokea taarifa za CAG halafu kusiwe na taarifa za utendaji wa ZAECA ya yalionekana kuwa na kasoro na wote waliotenda na kuthibitika kwa uhujumu wa uchumi wafikishwe katika mkono wa sheria. Alitaka Mamlaka hiyo kufanya kazi kwa pamoja na Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka DPP ili kupata matokeo mazuri na kuzielekeza taasisi hizo kutekeleza wajibu wao.

Alisema anataka hatua stahiki zichukuliwe kwa wanaoiba fedha za serikali ikiwamo Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB) kwa sababu kuna baadhi ya watu wakipokea fedha za kodi zinazolipwa na walipa kodi, lakini fedha haziingii katika akaunti.

Alimuahidi Mkurugenzi huyo mpya kumpa majina ya watu ambao walimtumia ujumbe kwamba walilipa ZRB na risiti wanazo na sasa wanadaiwa tena kwa kuwa fedha hazikufika katika bodi hiyo na mchezo huo ni wa siku nyingi na lazima utafutiwe ufumbuzi ili usiendelee. Eneo lingine ni Wizara ya Ujenzi Mawasiliano na Uchukuzi, alisema kuna fedha zilipelekwa kwenye kampuni ambazo hazipo na hazina usajili na kutaka lazima fedha hizo zipatikane na wahusika wachukuliwe hatua stahiki.

Alimtaka Mkurugenzi huyo kufanya kazi na ZAECA iongezewe uwezo wa kufanya kazi na kuhakikisha ina watu wenye weledi wanaotakiwa ili kupata matokeo.

"Katika utendaji wa ZAECA lazima kupata taarifa ya utendaji hadharani kwa vyombo vya habari ili kujua hatua zilizochukuliwa, watu wangapi wamechukuliwa hatua ni kesi ngapi zimefikishwa mahakamani na ngapi zimeshinda na ngapi zimekosa ushahidi," alisema.

Alivitaka vyombo vya sheria kufanya kazi za ziada ili kukomesha wizi na ubadhirifu wa mali za umma kwa sababu yakiendelea serikali itakosa kutekeleza ahadi ilizowaahidi wananchi katika kuleta maendeleo.

# Wadau habari wamkumbusha Waziri Nape kutimiza ahadi

**Na Mary Geofrey**

WADAU wa habari wamemtaka Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia, Nape Nnauye, kutimiza ahadi yake ya kuwasilisha mapendekezo ya wadau kuhusu mabadiliko ya sheria za habari katika mkutano wa bunge utakaoanza wiki ijayo jijini Dodoma.

Wito huo ulitolewa jana Dar es Salaam kwa niaba ya wanahabari na Wakili wa Kujitegemea, James Marenga, wakati akizungumza na vyombo vya habari.

Wakili Marenga aliyasema hayo ikiwa ni siku moja tangu Waziri Nape alipoahidi kuwa muswada wa sheria ya kulinda taarifa binafsi za kimtandao, unatarajiwa kuwasilishwa bungeni Septemba 13, mwaka huu.

"Wadau wangependa kuona ahadi ya Waziri Nape ya kupeleka mabadiliko ya sheria ya huduma za habari yanafanikiwa kwenye Bunge hili la Septemba, mwaka huu, ili mchakato wa mabadiliko hayo ukamilike," alisema Marenga.

Alisema mjadala wa serikali na wadau wa habari ulihusu Sheria ya Huduma za Habari 2016 na kwamba, kuna baadhi ya vipengele tayari wamekubaliana.

"Mjadala wa serikali na wadau ulihusu Sheria ya Huduma za Habari ya mwaka 2016 na yalijadiliwa ni mapendekezo ya wadau na yale ya serikali. Kuna vipengele tulikubaliana na vingine bado vipo kwenye mjadala," alisema Marenga.

Akizungumzia sheria ya kulinda taarifa binafsi za kimtandao, Marenga alisema sheria hiyo si ya wadau wa habari pekee bali inahusu watu wote.

"Halafu hii sheria ya 'data protection' (ulinzi wa taarifa binafsi) si kwa ajili ya wadau wa habari pekee ni sheria muhimu kwa watu wote," alisisitiza.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Huu udanganyifu wa tozo za maegesho haukubaliki

**KUMEKUWA** na malalamiko kwa baadhi ya watu wanaomiliki magari kubambikiwa tozo ya maegesho na kampuni inayotoa huduma hiyo jijini Dar es Salaam.

Malalamiko hayo yanatokana na wamiliki hao kudai kudaiwa tozo ya maegesho bila magari yao kuegesha sehemu zinazodaiwa kuwa yaliegeshwa.

Mmoja kati wa wamiliki wa magari alidai kuwa gari lake lilikuwa ndani kwa kipindi cha mwezi mmoja alipokuwa safari, lakini wakati likikaguliwa na Askari wa Usalama Barabarani, lilikutwa na deni na maeneo ambayo halijawahi kuegeshwa.

Mmiliki huyo akithibitisha hilo alisema pengine angekuwa ameacha ufunguo nyumbani, angeweza kusema mtu alilichukua na kwenda nalo huko linakodaiwa kuegeshwa. Lakini alisema aliliegesha ofisini na ufunguo kuondoka nao.

Huyo ni kati ya baadhi ya wamiliki wa magari wanaolalamika kubambikiwa tozo hizo ilihali magari yao hayajawahi kuegeshwa sehemu husika zinazodaiwa na wahudumu hao.

Wakati suala hilo likifuatiliwa, kampuni husika ilikiri kutokea kwa udanganyifu huo na kuwatupia lawama wahudumu waliopewa kazi ya kukusanya tozo hizo.

Kampuni hiyo ilibaini kuwa wanachokifanya wahudumu hao ni udanganyifu wakati wakipiga picha magari na kisha kujaza namba za magari mengine ambayo hajawahi kuegeshwa sehemu hiyo ili kupata idadi ya magari mengi.

Lengo la kufanya udanganyifu huo ni kupata kamisheni nyingi kutokana na idadi ya magari wanayokusanya tozo.

Kwa kweli udanganyifu huu haukubaliki kwa sababu huo ni wizi kama ulivyo wizi mwingine ambao mhalifu akipatikana na hatia huchukuliwa hatua za kisheria.

Kimsingi kitendo cha kampuni iliyopewa dhamana na kukusanya tozo hizo inapaswa kuwachukulia hatua wahudumu wake ili tabia hiyo ikomeshwe.

Suala hilo pia liliibua Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC), na kuziagiza Halmashauri za Manispaa ya Temeke na Kinondoni, kuweka utaratibu mzuri wa tozo za maegesho ya magari ili kuondoa malalamiko kwa wananchi.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo alizishauri halmashauri hizo zikarejee na kuangalia vizuri utaratibu wa kukusanya tozo hizo.

Kamati hiyo imetaka wananchi wanufaike na huduma na sio kuumizwa kama ilivyolalamikiwa.

Kama kuna wahudumu wanaofanya udanganyifu na wamegundulika wanapaswa kuchukuliwa hatua mara moja kama wahalifu wengine ili wasiendelee kuharibu lengo na nia nzuri ya ukusanyaji wa tozo hizo.


Utaratibu wa kuchukua tozo kwa kupiga picha namba za magari uliwekwa ili kuepuka udanyifu uliokuwa ukifanyika awali wa kubandikiwa risiti kwenye kioo cha gari na pesa hizo kutofika sehemu husika.

Utaratibu wa sasa unaruhusu mtu mwenye gari kulipa mojamoja kupitia mtandao anapopewa namba maalumu ya kulipa na kuepusha udanganyifu wa mapato.

Lakini, kama baadhi ya wahudumu wamegundua njia ya kuchakachua utaratibu huo kwa kuingiza namba za magari wanazozipiga picha na kisha kubambikia tozo ni jamba ambalo halipaswi kufumbiwa macho.

Kampuni iliyopewa jukumu hilo lazima ichukue hatua kuhakikisha suala hilo linakemewa kwa kuchukuliwa hatua madhubuti ili watu wengine wasitumie mwanya huo kuingiza dosari nia nzuri iliyowekwa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Wavuvi wafikiwe na fursa hii, kutimiza azma ya serikali



Na Mary Geofrey

**HIVI** karibuni Wizara ya Mifugo na Uvuvi, ilitia saini mkataba wa utekelezaji wa mradi wa ununuzi wa boti za uvuvi na vizimba vya kufugia samaki kati ya wizara ya mifugo na uvuvi (sekta ya uvuvi) na Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB), Jijini Dodoma.

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, akizungumza wakati wa kusaini makubaliano hayo, alisema serikali imeandaa mpango wa kuwawezesha wavuvi na wakuzaji viumbe maji kwa kuwapatia mitaji ili waweze kuboresha shughuli zao.

Mpango huu ni sehemu ya utekelezaji wa maelekezo aliyoyatoa Rais Samia Suluhu Hassan, katika hotuba yake ya Januari 7, mwaka huu, katika kilele cha Matembezi ya Miaka 58 ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Ndaki anasisitiza kutumika kwa fursa zilizopo katika kukuza Uchumi wa Buluu ikiwamo uvuvi na ukuzaji viumbe maji.

Aidha, itakumbukwa kuwa, Rais Samia Suluhu Hassan, wakati akifunga Maonyesho ya Sherehe za Wakulima (nanenane), Agosti 8, mwaka huu, aliagiza wizara hiyo, kuhakikisha kuwa uzalishaji wa Samaki unaongezeka kutoka tani 497,567 na kufikia tani 600,000 ifikapo mwaka 2025.

"Katika utekelezaji wa maelekezo ya Rais, wizara hii imeandaa mpango wa kuwawezesha wavuvi na wakuzaji viumbe maji kwa kutoa mikopo isiyo na riba kwa vyama vya ushirika, vikundi vya wavuvi, wakuzaji viumbe maji, wavuvi binafsi na makampuni ya wavuvi," anasema Ndaki.

Anasema kuwa mikopo hiyo itahusisha zana za kisasa za uvuvi ikiwamo boti, nyavu, injini, vizimba, vifaranga vya samaki, chakula cha samaki na pembejeo za ukulima wa mwani.

Ndaki anatoa wito kwa wavuvi na wakuzaji viumbe maji kuchangamkia fursa hiyo ya mikopo ili kuwanufaisha na kuzisihi halmashauri katika maeneo ya mradi kwenda kuwahamasisha wananchi wake ili kuitumia fursa hii ipasavyo.

Itakumbukwa kuwa, Rais Samia alitoa Sh. bilioni 60 kwa ajili ya kuendeleza sekta ya uvuvi, fedha ambazo zipo katika bajeti ya mwaka 2022/23.

"Endapo Fedha tulizopewa Sh. bilioni 60 zikitumika vizuri upo uwezekano mwaka ujao wa fedha hizo zikaongezeka," anasema Ndaki.

Waziri Ndaki alisema mradi huo unatakiwa kutekelezwa kwa muda maalum, hivyo ifikapo Juni 30, 2023 utekelezaji wa mradi huu uwe umekamilika.

Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, alikuwa miongoni mwa walioshiriki hafla hiyo na anatoa rai benki ya maendeleo kuongeza kasi ya utoaji mikopo.

"TADB inayo kazi kubwa ya kufanya ili kuhakikisha kwamba mikopo inafika kwa walengwa, kwa sababu watu wengi wamehangaika kupata mikopo hasa wavuvi wadogo na kusababisha kukata tamaa na kuacha kufanya shughuli za uvuvi," anasema Ulega.

Katibu Mkuu anayesimamia Sekta ya Uvuvi, Dkt. Rashid Tamatamah anasema boti hizo zina urefu wa mita saba hadi 14 zikiwa na injini zenye uwezo wa nguvu za farasi 9.9 hadi 60.

Alisema boti hizo zitakuwa na uwezo wa kubeba wavuvi sita hadi 20, kubeba Samaki tani 1.5, mtambo wa kufuatilia/kutambua uwapo wa Samaki (Fish finder), kifaa cha kuongoza boti (GPS), vifaa vya kuokolea maisha na zana za uvuvi zikijumuisha mishipi na nyavu. Jumla ya shilingi bilioni 11.5 zimetengwa kwa ajili ya kukopeshwa na mkopo huo utalipwa kwa muda wa miaka mitano bila riba.

Wizara pia itatoa mkopo kwa wafugaji samaki kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya kujenga jumla ya vizimba 831 na kila kimoja kitakuwa na ukubwa wa mita za ujazo 144 M3 - 256 M3. Vilevile, itatoa jumla ya vifaranga 4,080,000 na chakula cha Samaki tani 3,482.5.

Aidha, mkataba huo uliosainiwa utahusisha wakulima wa mwani ambapo jumla ya wakulima 821 watakopeshwa kamba 108,372, tai 7,152,552 pamoja na mbegu za mwani. Kwa ujumla kiasi cha shilingi bilioni 21 zitatumika kwa ajili ya vizimba na zao la mwani.

Hii ni fura kwa Watanzania ambao wamejikita kwenye sekta ya uvuvi kwanza kabisa kutambua fursa iliyopo kupitia fedha zilizotolewa na serikali.

Wakulima wahamasishane kuhusu fursa hii ili wale walengwa ndio wanufaike kwa ajili ya kutimiza lengo la serikali la kuinua sekta ya uvuvi. Haitapendeza kama wavuvi ambao ndio walengwa wasifikiwe na wafikiwe watu ambao hawapo kwenye sekta hiyo kwa malengo la maslahi ya watu binafsi.

Hii itakuwa ni kudhoofisha juhudi kubwa zinazofanywa na serikali za kukuza uchumi wa taifa letu hasa ule wa buluu.

Naamini watakaokuwa na wajibu wa kusimamia na kufikia walengwa watakuwa waadilifu na wazalendo katika kufanikisha hili.

Lakini pia wavuvi watakaofikiwa na mradi huu, kufanya kazi kwa uadilifu ili kufikia malengo ya serikali ili kupata kile ambacho serikali imedhamiria.

HABARI KITAIFA

# TCRA yataka ulinzi wa watoto ukatili, unyanyasaji mitandaoni

**Na Frank Monyo**

MAMLAKA ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) imesema pamoja na sheria zinazowalinda watoto dhidi ya unyanyasaji na udhalilishaji, ikiwamo Sheria ya Makosa Mtandaoni ya 2015, jamii inapaswa kushiriki kikamilifu kulinda kundi hilo dhidi ya ukatili kwenye mtandao.

Ofisa Mawasiliano Mwandamizi Mkuu wa TCRA, Semu Mwakyanjala, alisema hayo jana alipokuwa akizungumza katika kipindi cha Kumepambazuka kinachorushwa na kituo cha Radio One, Dar es Salaam.

Alisema ili kuwalinda watoto dhidi ya ukatili mtandaoni, jamii inapaswa kuhusika wakiwamo watunga sera, asasi za kiraia, viongozi wa dini na mamlaka za usimamizi wa sheria.

Mwakyanjala alisema ukatili dhidi ya watoto mtandaoni unaweza kukoma ikiwa jamii itashirikiana kutokomeza matukio ya ukatili.

"Mambo ya kihalisia katika ulimwengu wetu hayapo tofauti na yale yanayotendeka kwenye mifumo ya mtandao, hivyo ikiwa tunawalinda watoto dhidi ya ukatili kwenye ulimwengu wa kawaida, vivyo hivyo tuwajibike kuwalinda katika mazingira ya kimtandao na kwenye mifumo yote ya mawasiliano," alisisitiza Mwakyanjala.

Aliongeza kuwa umuhimu wa waandaaji wa maudhui mtandaoni pamoja na waundaji wa mifumo ya mawasiliano inayobeba maudhui kuhakikisha wanaweka miundombinu inayowalinda watoto wakati wanapolazimika kuingia kwenye mitandao kwa shabaha ya kujifunza na kupata elimu.

"Waandaaji maudhui wanatakiwa wahakikishe maudhui wanayotengeneza yanakuwa yenye staha, yasiwe yenye kuhamasisha ukatili dhidi ya watoto," alisema.

Shirika la Umoja wa Mataifa la Watoto (UNICEF) linabainisha kuwa ukatili dhidi ya watoto umekuwa ukiongezeka hasa miongoni mwa watoto wa kike.

Sheria ya Makosa ya Mtandao ya 2015 kifungu cha 13 inatoa katazo la kuchapisha ponografia za watoto kwenye mifumo ya kompyuta, aina ya ukatili ambapo UNICEF inasema umekuwa ukiongezeka kwa kasi kwenye mazingira ya mtandao.



Diwani wa Kata ya Kivukoni, Sharik Choughule, akizungumza katika kikao cha Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam juzi, ambapo aliiomba halmashauri hiyo, kujenga ofisi ya ofisa mtendaji wa kata hiyo. **PICHA: JUMANNE**

# RC ataka uhakiki kodi wawekezaji

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

MKUU wa Mkoa wa Pwani, Abubakar Kunenge, amesema kuna haja ya kuhakiki kampuni zilizowekeza katika mkoa huo ili kujiridhisha kama zinalipa kodi.

Pia ameitaka Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kwenda katika viwanda kufuatilia ulipaji wao wa kodi na sehemu zinazolipiwa.

Kunenge aliyasema hayo jana katika kikao cha kufanya tathmini ya utekelezaji wa bajeti mwaka wa 2021/22 na mkataba wa Lishe pamoja na Miongozo ya Elimu na ukusanyaji wa mapato katika mkoa.

Kwa mujibu wa Kunenge, hali ya ukusanyaji wa kodi haiendani na uwekezaji uliofanyika katika mkoa wa Pwani, hivyo akasema tathmini hiyo itabainisha tatizo lilipo.

Mkuu huyo wa mkoa alisema ili kukuza uchumi wa mkoa na kuleta mabadiliko ya kimaendeleo, ni lazima kudhibiti mianya ya upotevu wa mapato pamoja na ukwepaji kodi kwa wafanyabiashara na wawekezaji.

Awali akizungumza katika kikao hicho, Katibu Tawala wa Wilaya ya Bagamoyo, Kasilda Mgeni, alisema kuna baadhi ya kampuni zinafanya shughuli katika Halmashauri ya Chalinze lakini kodi zinalipa mkoa mwingine.

Mgeni alisema baadhi ya kampuni hizo zimekuwa zikienda kulipa kodi mahali zinakopenda kupeleka bidhaa zao.

"Serikali iingilie kati ili ushuru ukusanywe kwa usawa na maeneo haya kampuni zinakozalishia yanufaike badala ya utaratibu wa baadhi yao wanavyofanya kwa sasa," alisema Mgeni.

Katibu tawala huyo alisema barabara zinaharibika na Wakala wa Barabara Mjini na Vijijini (TARURA) haina bajeti ya kutosha, hivyo kodi hizo zikisimamiwa vizuri zitaondoa changamoto hizo.

# Raia 82 Ethiopia mbaroni kwa madai kuingia nchini bila vibali

**Na Friday Simbaya,** IRINGA

JESHI la Uhamiaji Tanzania (UT) Mkoa wa Iringa kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi, limewakamata raia wa Ethiopia 82, dereva mmoja na msaidizi wake raia wa Tanzania kwa madai ya kuingia nchini bila kibali na kusafirisha wahamiaji haramu.

Ofisa Uhamiaji Mkoa wa Iringa, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Uhamiaji (SACI) Agnes Luziga. Aliwaambia waandishi wa habari jana kuwa watuhumiwa wote wamekamatwa katika eneo la Tosamaganga, Barabara ya Iringa-Mbeya wilayani Iringa na kikosi maalum cha askari wa uhamiaji wakati wakitekeleza majukumu yao ya kila siku. Alisema baada ya mahojiano, watuhumiwa wote walibainika walikuwa wakitokea nchini Kenya kupitia Hololi mkoani Kilimanjaro na Dodoma kwenda Mbeya kwenye gari namba T 743 CYP aina ya Mitsubishi Fuso wakienda Mbeya na baadaye Afrika Kusini kupitia Malawi.

"Jeshi la Uhamiaji Mkoa wa Iringa limewakata raia wa Ethiopia 82 kwa tuhuma za kuingia nchini bila kibali pamoja na raia wa Tanzania wawili kwa madai ya kufanya biashara ya kusafirisha wahamiaji haramu," alisema Luziga.

Alisema watuhumiwa wote raia ya Ethiopia, wanatarajia kufikishwa mahakamani kwa kusafirisha wahamiaji haramu na kuongeza kuwa watuhumiwa wanashikiliwa chini ya Sheria ya Uhamiaji Sura 54, marejeo mwaka 2016 pamoja na kanuni zake.

Kutokana na kukithiti kwa wahamiaji haramu nchini, aliwataka wananchi kuendelea kutoa ushirikiano kwa kutoa taarifa wanapomtilia mtu shaka katika mazingira yao.

Alisema kikundi maalum cha doria mkoa wa Iringa na wilaya zake kinaendelea na jukumu lake la saa 24 kuwasaka na kuwakamata watu wote wanaojihusisha na biashara ya wahamiaji haramu.

"Biashara hii ni hatari kwa usalama wa nchi yetu na jukumu la usalama ni letu sote hivyo tushirikiane," alisema.

# Mtumishi kutoka Sumbawanga apewa cheo kinachoogopwa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KAMATI ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC), imepongeza Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kwa kupeleka Mkuu mpya wa Kitengo cha Ununuzi katika Halmashauri ya Mji wa Tunduma akitokea Sumbawanga kutokana na kila aliyeteuliwa kushika nafasi hiyo katika miaka ya karibuni, kufariki dunia na kusababisha kitengo hicho kuogopwa.

Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Selemani Zedi, alitoa pongezi hizo jana ya kufanya mahojiano na uongozi wa halmashauri hiyo kuhusu hoja za ukaguzi za mwaka 2020/21.

Alisema taarifa ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) ilionyesha kulikuwa na udhaifu mwingi kwenye eneo la ununuzi ambapo Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo alidai kuwa idara ya ununuzi ilikuwa haina mtaalamu wa ununuzi.

"Mtu wa ununuzi wa kwanza aliyekuwapo alifariki dunia, akaja mwingine wa pili akafariki dunia, akaja mwingine wa tatu akafariki dunia, ikalazimu wamchukue mwalimu wa kawaida wa sekondari kusimamia ununuzi, sasa huyu mwalimu alikuwa hana utaalamu ikasababisha idara hii ikawa na upungufu mwingi sana," alisema.

Alitaja upungufu uliyobainika kuwa ni pamoja na wazabuni kupewa kazi wakati hawajaidhinishwa na Wakala wa Ununuzi wa Serikali na vifaa vinalipiwa lakini havipokewi.

"Sheria ya Ununuzi inasema ukitangaza kazi, waombaji wanaoomba kazi ya kufanya, unamchagua aliyetaja bei ndogo kuliko wote, walikuwa hawatekelezi hilo takwa, waliokuwa wakiomba wanampa kazi mtu aliyetaja bei kubwa," alisema.

Aliongeza kuwa pia walikuwa wanafanya malipo kwa makandarasi wakati hawajawasilisha ile bidhaa na utaratibu unataka asilipwe hadi bidhaa ipokewe.

"Kamati inampongeza mkurugenzi baada ya kuona kitengo muhimu kinaendeshwa na mwalimu wa kawaida akafanya mawasiliano na TAMISEMI na wao wakamtafuta Ofisa Ununuzi mwenye utaalamu kutoka Sumbawanga na kupelekwa hapo, tangu apelekwe tatizo lililokuwapo limekwisha na sasa ununuzi unakwenda vizuri," alisema.

# Majaliwa ang'aka kibanda mlinzi kugharimu mil. 11/-

**Na Mwandishi Maalum,** UYUI

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amemwagiza Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Tabora, Musa Chaulo, kuwakamata watu wote wanaohusika na usimamizi wa ujenzi wa Chuo cha Ufundi Stadi (VETA) wilayani Uyui mkoani Tabora kwa tuhuma za ubadhirifu wa fedha za mradi huo.

Ameagiza hatua hiyo baada ya kukagua mradi huo na kuonyesha kutoridhika na gharama za ujenzi wa baadhi ya majengo, kikiwamo kibanda cha mlinzi ambacho ujenzi wake umegharimu Sh. milioni 11.

"Sitamvumilia yeyote atakayemhujumu Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan, watafutwe na wachukuliwe hatua," Majaliwa aliagiza jana baada ya kukagua mradi wa ujenzi wa chuo wilayani hapa.

Alisema hajaridhishwa na ujenzi wa chuo hicho ambacho majengo yake yanejengwa kwa gharama kubwa tofauti na uhalisia kwa kutumia mfumo wa nguvu kazi ya ndani (force account).

Mbali na ujenzi wa kibanda cha mlinzi, Waziri Mkuu pia alionyesha kutoridhishwa na ujenzi wa nyumba za watumishi chuoni huko ambao nyumba moja yenye uwezo wa kuchukua familia mbili inajengwa kwa gharama ya Sh. milioni 114 na tayari wameshatumia zaidi ya Sh. milioni 70 na haijakamilika.

"Nyumba moja yenye uwezo wa kuchukua familia tatu Wizara ya Afya inajenga kwa Sh. milioni 90 na Ofisi ya Rais (TAMISEMI) wanajenga nyumba za walimu zenye uwezo wa kuchukua familia mbili kwa gharama ya Sh. milioni 57 na wanajenga kwa mfumo wa force account kama mnavyojenga hapa, hii haikubaliki," alisisitiza.

Kutokana na kutoridhishwa na ujenzi wa chuo hicho unaosimamiwa na VETA, Majaliwa amemwagiza Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Balozi Dk. Batilda Burian, asimamie ujenzi wa chuo hicho ili ukamilike kwa wakati.

"Mkuu wa mkoa simamia vizuri ujenzi wa chuo hiki, tunataka ukamilike kwa wakati," Waziri Mkuu aliagiza.Majaliwa alisema ujenzi wa vyuo hivyo unatokana na maono mazuri ya Rais Samia kwa lengo la kuwawezesha vijana kupata ujuzi utakaowawezesha kujiajiri au kuajiriwa na hatimaye kupunguza shida ya upatikanaji wa ajira nchini.

"Kila siku Mkuu wa Nchi anawasisitiza watanzania juu ya matumizi mazuri ya fedha za umma, waliohusika wote wachukuliwe hatua," aliagiza.

Awali, Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa VETA, Anthony Kasore, alisema ujenzi huo unaotarajiwa kugharimu Sh. bilioni 2.9 ukihusisha jumla ya majengo 17 ambayo ni jengo la utawala, majengo manne ya karakana, madarasa mawili makubwa, mabweni mawili, nyumba mbili za watumishi, jengo la umeme, jengo la bohari na jengo la ofisi ya mlinzi.Alitaja fani zitakazokuwa zinatolewa baada ya kukamilika kwa chuo hicho ni uhazili na kompyuta, ubunifu wa mitindo, uashi, umeme wa majumbani, ufundi wa magari, uchomeleaji na uungaji vyuma, ufugaji wa samaki, matumizi ya kompyuta, usindikaji wa mazao ya nyuki, mapambo na kutengeneza bidhaa za batiki, kilimo cha mboga na udereva.

Katika ripoti yake ya ukaguzi kwa mwaka 2020/21 iliyowasilishwa bungeni Aprili 12 mwaka huu, CAG Charles Kichere, mbali na mambo mengine, amebainisha kuwapo shida katika utekelezaji wa miradi ya VETA nchini.



Mtaalamu wa Mazoezi Tiba wa Hospitali ya Taifa Muhimbili, Twarib Mussa (kulia), akimpa maelezo, Sharifa Ramadhan, kuhusu matibabu anayotakiwa apatiwe mtoto wake Feisal Hamis, katika kambi ya siku tatu ya matibabu bure hospitalini hapo, jijini Dar es Saaam jana.
**PICHA: JUMANNE JUMA**

# Kampuni 200 zabainika kutolipa ushuru huduma

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KAMPUNI zaidi ya 200 za uwindaji katika Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti mkoani Mara zimebainika kutolipa ushuru wa huduma, hivyo kusababisha kuzorotesha mapato.

Kutokana na hali hiyo, halmashauri hiyo imeagizwa kuhakikisha ushuru huo unakusanywa ili ipate mapato stahiki.

Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC), Selemani Zedi, alibainisha hayo jana baada ya kuhoji halmashauri hiyo kuhusu hoja za ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2020/21.

Alisema kampuni hizo zimekuwa hazilipi ushuru ambao zinapaswa kuulipa kwa mujibu wa sheria kutokana na kufanya shughuli za uwindaji.

Alifafanua kuwa sheria inasema kama uwindaji unafanywa ndani ya halmashauri fulani, asilimia 20 ya mapato yanatakiwa yabaki ndani ya halmashauri hiyo.

Zedi alisema Serengeti imebainika kuwa na uzembe kwa kuwa haifuatilii mapato hayo na hivyo kushindwa kupata mapato ambayo inastahili kuyapata.

"Kosa kubwa ambalo Wilaya ya Serengeti walilifanya, sheria inasema kwamba ipate asilimia 20 ya mapato ya uwindaji, sasa hawa wameshindwa kufuatilia kuyajua hayo mapato ya uwindaji ili wapige hesabu asilimia yao ni shilingi ngapi.

"Kwa hiyo, walitakiwa wafanye jitihada kwenda kwenye mamlaka husika kama Wizara ya Maliasili na Utalii au Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ili wakapewe takwimu zinazoonyesha kwamba uwindaji Serengeti umeingiza shilingi ngapi ili wapatiwe asilimia 20 yao," alisema.

Makamu Mwenyekiti huyo pia alisema shida hiyo iko katika kodi ya mapato ya hoteli, akibainisha kuwa Mbuga ya Serengeti ina hoteli nyingi za kitalii ambazo zinapaswa kulipa ushuru kutokana na mapato ya vinywaji, malazi na mambo mengine lakini menejimenti iliyokuwapo ilishindwa kufuatilia.

"Hata kujua kwamba ndani yake kuna hoteli ngapi zinafanya biashara kwa kiasi gani ili na wao wapige hesabu ya ushuru wao, hawakufanya. Kwa hiyo, kamati imemwagiza mkurugenzi na timu yake kuongeza jitihada na kufanya kazi kwa mujibu wa sheria ili Serengeti inufaike na mapato kwa kuwa haistahili kuwa maskini kwa sababu ndani yake kuna shughuli kubwa za uwindaji ambazo zingeipatia mapato,"alisema.

## HABARI KITAIFA

# AZAKI kujadili mbinu na fursa za maendeleo

**Na Mwandishi Wetu**

WASHIRIKA wa maendeleo zaidi ya 500 wa sekta ya umma na binafsi kutoka Tanzania, Uganda na Kenya, wanatarajia kushiriki Wiki ya Asasi za Kiraia (AZAKI), itakayofanyika jijini Arusha mwezi ujao.

Mratibu wa Wiki ya AZAKI 2022, Dk. Shirley Mushi, alisema hayo jijini Dar es Salaam juzi na kufafanua kuwa usajili wa ushiriki kwa mwaka huu utafanyika kwa njia ya mtandao na kuwataka washiriki wajiandikishe mapema ili kupata nafasi.

"Tumefungua rasmi usajili wa wiki ya AZAKi kwa njia ya mtandao, hivyo tunaowamba wadau watembelee tovuti yetu csoweek.info, kwa ajili ya kujiandikisha, ili kushiriki tukio hili muhimu," alisema Dk. Mushi.

Alifafanua kuwa Wiki ya AZAKi 2022 itafanyika Oktoba 24 hadi 28 mwaka huu, na kwamba itawapa kipaumbele wananchi katika kila shughuli na mijadala itakayofanyika, huku ikionyesha mbinu, ufanisi na ubunifu wa sekta hiyo kama mdau muhimu wa maendeleo.

Dk. Mushi alisema Kamati Tendaji ya Wiki ya AZAKi 2022 na waandaaji walizindua rasmi shughuli hiyo, yenye kaulimbiu 'Maendeleo ya Watu, Simulizi za Watu' inayosisitiza kwamba, watu ndio sehemu kuu ya malengo ya AZAKi, na uwepo wake.

"Kauli mbiu hii inaruhusu kutafakari kwa kina juu ya mbinu, mifumo na michakato mingi inayotumiwa na AZAKi kutatua vikwazo ambavyo Watanzania wanakabiliana navyo. Pia inathibitisha dhamira ya AZAKi na wadau wa maendeleo katika kuleta mabadiliko," alisema.

Aliongeza kuwa ajenda ya Wiki ya AZAKi 2022 itaelekezwa, kwa ajili ya kuhakikisha watendaji wa sekta mbalimbali wanaimarisha ushirikiano na mahusiano yanayolenga kuleta maendeleo.

"Kimsingi, wiki hii inawaleta pamoja wadau wakuu wa maendeleo na inalenga kuimarisha mahusiano na ushirikiano kati ya wadau wakuu wa maendeleo, kutatua vikwazo vikubwa vya maendeleo, kuzalisha na kubadilishana mawazo yanachochea juhudi za maendeleo," alisema.

# Wadau waipa kongole serikali kushuka mafuta

**Na Waandishi Wetu**

SIKU moja baada ya serikali kutangaza kushuka kwa bei za mafuta ya petroli, mafuta ya taa na dizeli, wadau wa usafirishaji wamepongeza uamuzi huo wakisema itasaidia kupunguza mfumuko wa bei.

Juzi Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), ilitangaza bei za ukomo wa mafuta kwa mwezi Septemba ambazo zimeanza kutumika jana zikionyesha petroli itauzwa Sh. 2,969, dizeli Sh. 3,125, bei hizo ni kwa ajili ya Jiji la Dar es Salaam.

Wakizungumza na Nipashe kuhusu nafuu hiyo, wadau mbalimbali walisema hatua hiyo ni nzuri ambayo itawapunguzia mzigo wananchi ununuzi wa bidhaa.

Mfanyabiashara wa mafuta ya petroli na dizeli jijini Mwanza, Jamal Babu, alipongeza serikali kwa kushusha bei ya bidhaa hiyo kwa wananchi wanaonunua rejareja.

Alisema hatua hiyo itasaidia kupunguza mfumko wa bei kwa bidhaa mbalimbali zikiwamo za shambani.

Aliwataka wafanyabiashara wenzake kufuata sheria na maelekezo ya serikali ya kushusha bei ya mafuta na kuhakikisha wanauza kwa bei elekezi.

Babu, ambaye pia ni Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) mkoani Mwanza, alisema uamuzi huo wa serikali umekuja wakati mwafaka na wananchi wanatakiwa kutumia fursa hiyo kujenga uchumi wao kwa mtu mmoja mmoja.

Alisema, serikali imeamua kuwasaidia wananchi wake kwa kuweka ruzuku ya Sh. bilioni 100, kila mwezi kuhakikisha bei inapungua ili wananchi waweze kumudu kununua mafuta na kueleza kuwa sio jambo dogo kama watu wanavyofikiria.

Mfanyabiashara wa mabasi ya abiria ya Movement Class yanayofanya safari zake kati ya mikoa ya Kilimanjaro na Arusha, Abel Lena, alisema kushuka kwa bei ya mafuta kumepunguza machungu ya kuhudumia magari wanayomiliki kutokana na gharama za uendeshaji kuwa kubwa.

"Kama mafuta yameshuka, tunatamani miezi inayokuja yashuke zaidi ya sasa, itatusaidia ikiwa hali itakuwa hivyo. Hata abiria tunaobeba, kila mmoja analia kwamba maisha yamekuwa magumu, wanaomba punguzo la nauli.

"Hii ndiyo ahueni tunayohitaji ili kuleta usawa, kati ya ukuaji wa kiuchumi na kulenga mfumuko wa bei na utulivu wa fedha."

Mwakilishi wa Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF), Mkoa wa Dodoma, Ringo Ilingo, alisema kushuka kwa bei ya mafuta kutasadia kupunguza ukali wa maisha kwa wananchi.

Alisema, Tanzania bado inahitaji mafuta katika shughuli zake mbalimbali za kiuchumi, hivyo kitendo cha bei za mafuta kuwa juu kinasababisha athari kwa wananchi.

Katibu wa Wajasiriamali Mkoa wa Dodoma, Christopher Dioniz, alisema kushuka kwa bei ya mafuta kunawasaidia kupunguza mzigo mkubwa wa gharama za usafirishaji wa bidhaa zao.

Mwenyekiti wa Chama cha Wamiliki wa mabasi yanayofanya safari kati ya Jiji la Mbeya na Mji wa Tunduma mkoani Songwe, Bob Mwampashe, alisema kushuka kwa bei ya mafuta kutasaidia kuimarisha uhusiano kati ya wamiliki hao na wafanyakazi.

Alisema baadhi ya wamiliki wa mabasi waliamua kubadili uwekezaji kwa kuuza mabasi baada ya biashara ya usafirishaji kuwa ngumu na baada ya kutangazwa bei mpya sekta hiyo itaimarika.

Aidha, wafanyabiashara Kanda ya Ziwa wametakiwa kufuata agizo lililotolewa na serikali kuhusu kushuka kwa bei ya mafuta hapa nchini.

Akizungumza na Nipashe Meneja wa EWURA Kanda ya Ziwa, George Mhina, alisema ni kosa kwa mfanyabiashara kukaidi agizo la serikali la kushusha bei kama ilivyotangazwa.

Alisema kutokana na mabadiliko hayo ambayo yamechangiwa na soko la dunia na ruzuku ambayo serikali inatoa ya Sh. billion 100 ya kila mwezi wananchi wa Kanda ya Ziwa watanufaika.

Aliwataka wafanyabiashara wote wa vituo vya mafuta kuzingatia agizo hilo lililotangazwa na waweke mabango yao kwenye vituo vyao ili kuonyesha mabadiliko ya bei.

Denisi Ndibyalema, dereva wa daladala jijini Mwanza alisema wamelipokea kwa furaha tangazo hilo kwa sababu mafuta yalipopanda kwa asilimia kubwa faida ilikuwa ndogo au wakati mwingine hamna kabisa hivyo aliomba bei hiyo iendelee kushuka zaidi ili waweze kupata faida katika biashara zao.

"Bei za mafuta hizi zingekuwa za kudumu ingekuwa vizuri badala ya kubadilika badilika kila wakati, leo tunaweza kushangilia lakini baada ya mwezi mambo yakabadilika tena ikawa hali siyo hali," alisema Ndibyalema.

■**Imeandaliwa na Richard Makore (Mwanza), Godfrey Mushu (Arusha), Paul Mabeja (Dodoma), Nebart Msokwa (Mbeya)**



Wataalamu na maofisa wa ubalozi wa Tanzania nchini Uholanzi, wakiongozwa na Waziri wa Nishati, January Makamba (wa pili kushoto), wakijadiliana na Makamu wa Rais anayeshughulikia miradi ya LNG, Cederic Cremers (kulia), nchini Uholanzi juzi kuhusu utekelezaji wa mradi wa gesi ya LNG. Waziri Makamba, alimwakilisha Rais Samia Suluhu Hassan kwenye mkutano wa mabadiliko ya tabia nchi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waziri January ateta na wakuu Shell mradi LNG

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Nishati, January Makamba, ametembelea ofisi za Kampuni ya Shell nchini Uholanzi na kuzungumza na viongozi wakuu wa kampuni hiyo kuhusu masuala ya utekelezaji wa mradi wa LNG nchini.

Katika mazungumzo hayo na Makamu wa Rais anayeshughulikia miradi ya LNG, Cederic Cremers, Makamu wa Rais wa Shell anayehusika na uhusiano wa serikali, John Crocker, Waziri Makamba alielezea azma ya Rais Samia Suluhu Hassan, kuhakikisha mazungumzo yanakamilika mwezi Desemba mwaka huu na hatua za utekelezaji zinaanza haraka.

Katika mikutano hiyo, Waziri Makamba pia alieleza mpango wa serikali wa kuanzisha Ofisi Maalumu ya Kusimamia Utekelezaji wa Mradi wa LNG (Tanzania LNG Office), mwezi Novemba mwaka huu kwa lengo la kuratibu, kuharakisha na kurahisisha hatua za utekelezaji wa mradi.

Mradi huo wa kuchakata na kusindika gesi asilia iliyogundulika katika bahari kuu Kusini mwa Tanzania, utaleta nchini uwekezaji wenye thamani ya Dola za Kimarekani bilioni 40, unatekelezwa na Kampuni ya Shell ya Uholanzi na Equinor ya Norway na washirika wao.

Waziri Makamba, alieleza kwamba mradi huo una manufaa mengi kwa Tanzania na utafungua fursa nyingi kwa wananchi wa mikoa ya Kusini mwa Tanzania, kuiongezea mapato nchi, kuleta ajira na mapinduzi ya kiuchumi na kijamii nchini.

Kwa upande wa Kampuni ya Shell, Crocker, aliishukuru Serikali ya Tanzania kwa kuwapa wawekezaji matumaini na kutoa kipaumbele katika mradi huo na kuwezesha kusainiwa kwa mkataba wa awali.

Pia, alieleza kuridhishwa na hatua ya majadiliano iliyofikiwa katika maandalizi ya utekelezaji wa mradi huo.

Aidha, Crocker alisisitiza nia yao na ya washirika wao ya kutekeleza mradi.

# Watendaji kikaangoni ukusanyaji mapato

Na Thobias Mwanakatwe, IKUNGI

HALMASHAURI ya Wilaya ya Ikungi mkoani Singida imeweka mkakati kwamba mtendaji yeyote atakayeonekana kulegalega katika ukusanyaji wa mapato kwenye eneo lake atafutwa kazi.

Mkakati huo ulitangazwa jana na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Justice Kijazi, kungwa mkono na madiwani wakati wa kikao cha kawaida cha Baraza la Madiwani.

Hatua ya Kijazi kutoa tamko hilo ilitokana na malalamiko ya madiwani kwamba baadhi ya maofisa watendaji wanakwepa kutumia mashine za kielektroniki (POS) katika ukusanyaji wa mapato.

Kijazi alisema katika mwaka wa fedha wa 2021/ 2022, halmashauri hiyo ilifikia asilimia 102 ya kukusanya mapato.

Hata hivyo, alisisitiza kuwa itakuwa haina maana kukusanya mapato kwa wingi na matumizi yakawa makubwa na kueleza kuwa wataondoa posho zisizo za lazima na fedha hizo watazielekeza kwenye miradi ya kupata fedha zaidi.

Alisema mafanikio ya kufikia asilimia hiyo yametokana na ushirikiano mzuri baina ya madiwani na watumishi wa kada zingine katika halmashauri hiyo na lengo likiwa ni kuiletea maendeleo.

Kijazi aliliomba baraza hilo la madiwani kupitisha Sh. milioni 100 kwa ajili ya kuifunga stendi ya mabasi ya Ikungi akitolea mfano stendi ya Manyoni ambayo kila siku wanakusanya Sh. milioni 3.5 mabasi yanapopita hivyo ikifunguliwa wanaweza kupata Sh. milioni tatu hadi nne.

Naye Diwani wa Unyahati, Abel Suri, alisema watendaji wote wa kata wawajibike na kuongeza bidii ya kukusanya mapato kwani hiyo ni moja ya kazi yao kubwa na hata katika mkataba wao wa kazi jukumu hilo lipo. Suri alisema moja ya kipimo cha utendaji kazi wa maafisa hao ni ukusanyaji wa mapato na si vinginevyo. Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi, Ally Mwanga, alisema halmashauri hiyo imeanza mkakati mpya wa kutafuta vyanzo vipya vya mapato wenye lengo la kuongeza mapato badala ya kutegemea chanzo kikubwa cha mazao ya biashara ambacho kimeporomoka kutokana na uhaba wa mvua.

"Tumekwishaingia mwaka mpya wa fedha na kama mnavyojua kuwa jiografia ya halmashauri yetu mvua zikinyesha chini ya kiwango zinasababisha mazao kupungua kama vile alizeti, mpunga, dengu na mazao mengine," alisema.

Alisema chanzo kipya cha mapato kitakuwa ni pamoja na kituo cha mabasi katika Kata ya Mungaa ambapo kama watasimamia vizuri ukusanyaji wa mapato baada ya magari kuingia katika stendi hiyo kwa mwezi watapata Sh. milioni 16.

Mwanga alisema maeneo mengine watakayo yaangalia ni stendi ya mabasi ya Isuna, Ikungi, Ihanja, Sepuka na maeneo mengine yanayofanana na hayo na kufungua minada Kijiji cha Choda na Chungu jambo ambalo litasaidia kwa kiasi kikubwa kuongeza mapato ya halmashauri hiyo.

Alisema kuacha magari yakipita bila ya kuweka utaratibu wa kuingia stendi zitakazoanzishwa itakuwa ni hasara kwa halmashauri hiyo ambapo alitumia nafasi hiyo kuziomba kila kata yanapopita magari hayo ni lazima watengeneze stendi hizo.

Mwanga alitaja vyanzo vingine wanavyotarajia kuvianzisha kuwa ni pamoja na kufungua minada maeneo mengine ndani ya halmashauri hiyo.

## Bil. 13/- kupunguza migogoro uhifadhi

Na Mwandishi Wetu

SERIKALI imepokea Euro milioni sita sawa na shilingi bilioni 13.2 kutoka Shirika la Ujerumani la GIZ kwa ajili ya mradi wa kupunguza migogoro baina ya binadamu na wanyamapori kwenye maeneo ya pembezoni mwa hifadhi.

Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mary Masanja, aliyasema hayo wakati wa ziara ya kikazi katika Chuo cha Mafunzo ya Maliasili kwa Jamii Likuyu, Sekamaganga, Namtumbo mkoani Ruvuma.

"Rais Samia Suluhu Hassan ametafuta Sh. bilioni 13.2 ambazo zitatumika katika kufanya utafiti wa maeneo yenye changamoto za wanyama wakali na waharibifu, kutoa elimu kwa jamii zinazoishi pembezoni mwa hifadhi kuhusu uhifadhi na kukabiliana na wanyama wakali na waharibifu," alisema.

Alisema mradi huo wa miaka mitatu una lengo la kutoa ujuzi kwa jamii kuhusu namna ya kukabiliana na wanyama wakali na waharibifu ambapo jamii hizo zitasambaza ujuzi kwa jamii zingine.

Pia alisema mafunzo hayo pia yatatolewa kwa askari wanyamapori wa vijiji (VGS) ili kuongeza nguvu ya kukabiliana na wanyamapori wakali na waharibifu.

Alisema endapo jamii zitapata uelewa wa namna ya kuhifadhi na kukabiliana na wanyama wakali na waharibifu hakutakuwa na chuki baina ya binadamu na shughuli za uhifadhi.

Naye Mkuu wa Chuo cha Mafunzo ya Maliasili kwa Jamii Likuyu Sekamaganga, Jane John, alisema chuo hicho kinatoa mafunzo ya askari wa wanyamapori wa vijiji, askari wa misitu wa vijiji, askari wanaosimamia fukwe za jamii, kozi kwa viongozi na wajumbe wa kamati za maliasili za vijiji, Astashahada ya Utalii na Waongoza Watalii pamoja na mafunzo ya kudhibiti wanyama wakali na waharibifu.



Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo (katikati) na Katibu wa NEC ya CCM Siasa na Uhusiano wa Kimataifa, Kanali mstaafu Ngemela Lubinga, wakipitia kitabu chenye machapisho ya Mkutano Mkuu wa kwanza mpaka wa 12 wa Chama cha Kikomunisti cha Vietman (CPV), baada ya kukabidhiwa na Balozi wa Vietnam nchini, Komredi Nguyen Nam Tien (kushoto), katika ofisi ndogo za makao makuu ya chama hicho, Lumumba, jijini Dar es Salaam, jana. **PICHA: ADAM MZEE**

# Wajawa vicheko kupata majisafi

Na Joseph Mwendapole

WAKAZI wa Mtaa wa Nyakasangwe Kata ya Wazo, Kinondoni mkoani Dar es Salaam, wameanza kunufaika na huduma ya majisafi na salama baada ya kutekelezwa kwa mradi mkubwa wa maji.

Mradi huo umetekelezwa na Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) kupitia mradi wa kutoka Makongo hadi Bagamoyo, kupitia ufadhili wa Benki ya Dunia.

Mhandisi wa Miradi Mkoa wa Kihuduma wa DAWASA Mivumoni, Pascal Salida, alisema juzi kuwa mradi huo mpaka kukamilika kwake, umegharimu Sh. bilioni 65.4.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Nyakasangwe, Anthony Mwandege, alisema wananchi wengi hawakuwa na huduma ya majisafi na maeneo yao yalikuwa na changamoto ya msukumo mdogo wa maji lakini sasa tatizo hili halipo tena.

Alisema wananchi wa mtaa wake wana furaha kubwa kwa kuwa wameondokana na adha ya kutumia maji ya chumvi pamoja na kutumia gharama kubwa kununua maji kutoka kwa wafanyabiashara binafsi.

"Eneo kubwa la Nyakasangwe linapata maji kwa mara ya kwanza kabisa jambo ambalo ni historia hapa kwetu. Lakini hata kwa kipande kidogo kilichokuwa kikipata huduma kwa. mgawo wa maji ambao haukuwa sawa sasa huduma imeimarika na upatikanaji wa maji ni wa uhakika," alisema.

Alitoa wito kwa wananchi kujitokeza kuunganishiwa huduma ya maji na kuahidi kuwa serikali ya mtaa italinda miundombinu hiyo na kupambana na yeyote atakayethubutu kujaribu kuiharibu.

"Kwa kushirikiana na DAWASA tutaweka mipango mizuri kwa pamoja ambayo kupitia hiyo kila mwananchi atalipia huduma ya majisafi kila mwezi kutokana na matumizi yake," alisema Siwema Salum, mmoja wa wanufaika wa maji hayo huku akiishukuru DAWASA kwa kutimiza ahadi yao na kuwapatia majisafi.

"Tumekuwa tukitumia maji kutoka bwawani ambayo si salama kwa afya zetu hata kidogo. Mifugo imekuwa ikiingia na kunywa maji katika bwawa hilo tulilolitegemea siku zote kwa maji. Sasa tunachota maji yanayotiririka bombani. Hii kwetu ni kama ndoto, hivyo tunaishukuru sana serikali kupitia DAWASA," alisema.

Alisema kwa sasa matumizi ya maji chumvi na maji yasiyo salama kutoka katika bwawa sara ni historia na kila mwananchi wa Nyakasangwe anafurahia huduma ya majisafi na wameahidi kulipia gharama zote za huduma.


Mhandisi Salida alisema kwa sasa kazi ya kuwaunganishia wananchi maji inaendelea na hakuna mwananchi atakayeachwa kupatiwa huduma ya maji safi.

"Katika mtaa huu tuna malengo ya kuzipatia maji zaidi ya kaya 250 na mpaka sasa zaidi ya kaya 80 zinapata huduma tayari. Niwahakikishie wananchi kuwa hakuna mwananchi atakayeachwa bila kupata huduma ya majisafi," alisema.

Salida alisema kuboreshwa kwa huduma ya majisafi mtaa wa Nyakasangwe kutamaliza mgawo wa maji uliokuwapo pamoja na kuwaunganisha wateja wengi wapya huku huduma ya maji ikitarajiwa kuwa bora na ya uhakika.

Alisema mradi wa kuboresha huduma ya maji kutoka Makongo hadi Bagamoyo unalenga kuboresha upatikanaji wa maji kwa wakazi 450,000 na umehusisha ujenzi wa matangi matatu yaliyoko Vikawe, Mbweni na Tegeta A yenye ujazo wa lita milioni tano kila mmoja yatakayotumika kupokea na kusambaza maji kwa wakazi hao.

Ukurasa 13




Karibuni ndugu mlioenda Kenya na somo kamili mlilojifunza huko

BUFE

IJUMAA SEPTEMBA 9, 2022

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA



**Kijiji aina yake cha ufugaji nyuki, asali yake inarinwa kiteknolojia**

Ukurasa 14

# Ulivyo uvamizi wa tembo shambani ukisambaratisha mkulima kijijini

**Na Halfani Chusi**

MTU akiwa katika kijiji cha Mgowelo kilichopo katika kata ya Nyanzwa wilayani Kilolo, mkoa wa Iringa, suala la kuvamiwa na tembo ni la kawaida, licha ya wanakijiji kupeleka malalamiko kila wakati kupata msaada serikalini dhidi ya wanyama hao hatari.

Ni muda mrefu wamekuwa wakidhuru na kuhatarisha usalama wa raia mahali hapo, wanachafua mazingira, kwa kiasi kikubwa wanaharibu mazao ya wakulima na kudondosha miti. Yote zao lake ni kupatikana hasara kubwa.

Kwenye mazao yao kijijini, imekuwa kawaida wakulima wengi wanapata hasara kila wanapokutana na wanyama hao na ndio kilio cha kila mkulima akilalama kuambulia kipato duni, huku mazao kama mahindi yananasambaratishwa kwa eneo kubwa pindi yanakaribia kukomaa.

Baadhi ya wakazi kijijini humo, sasa wanaamua kwenda kulala shambani hasa usiku, wakikoleza moto na kupiga ngoma muda wote kuwatishia tembo wasiingie shambani, maana inasemekana tembo wana tabia ya kuogopa moto na makelele, kwamba inawatesa mno.

Hapo ndipo umma nao unaamua kuja na rai ya haja ya serikali kuwekeza nguvu zaidi kuwaondolea wananchi wa kijiji hicho adha, kwani wengine wanaingia hofu hata kusita kulima kwa kuhofia hasara inayosababishwa na tembo.

Nipashe ilishuhudia shamba la mkulima mmoja katika kijiji hicho, Musa Ngogo, akilalamika namna



Baadhi ya mashamba ambayo yameathiriwa na nyendo za tembo katika kijiji tajwa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

tembo walivyomtia hasara ya mazao yake

"Miwa na ndizi vilikuwa vimestawi sana, siku moja usiku tembo walivamia shambani kwangu, wakaanza kula miwa na kuharibu migomba ya ndizi na mingine ilikuwa imebeba mikungu iliyokomaa tulipopeleka malalamiko serikalini,

"Walikuja watu kutoka maliasili wakaja wakakagua shamba langu na sikuwa peke yangu, wakatuambia tutakuja kulipwa, lakini mpaka leo zaidi ya miaka mitano hatujalipwa na wengine wamefilisiwa kabisa mali zao," anasimulia

Rai ya wananchi ni kwamba, serikali kupitia mamlaka husika, sasa inapaswa kutambua madhila yanayowafika wanakijiji wanaoteseka na kupoteza mazao shambani, kwa sababu wanahofu wakiwashambulia tembo hao, huenda sheria itawageuka.

Wanakijiji wanaainisha kwamba, mateso hayo yapo katika hali endelevu kila mwaka, hasa kipindi cha mavuno wamekuwa wakiingiliwa sana na tembo mashambani mwao.

**SERIKALI YA KIJIJI**

Mwenyekiti wa Kijiji, Bakari Mtarula, anaungana na kilio cha wananchi wake, akiomba kupelekwa askari kusaidiana na wanakijiji kuwadhibiti.

"Serikali inatakiwa ije kijijini hapa ijenge kabisa kituo, siyo kama vile wanavyokuja na kuondoka. Inatakiwa waweke kambi hapahapa, ili iwe rahisi kutusaidia wanapotokea tembo mashambani.

"Maana, kwa miaka mingi tumekuwa tukipiga kelele wanakuja askari lakini hawakai kwa muda mrefu kwa hiyo wakiondoka tu tembo wanaingia.

Pia, mbali na serikali kutuletea watu wa kupambana na tembo, tunaomba watu wa maliasili waje kutupatia elimu ya namna ya kukabiliana nao. Inawezekana hatujui namna ya kuwaepuka na ndio maana wanatusumbua, " anaeleza mwenyekiti huyo.

Anafafanua kuwa tembo hao wamekuwa waharibifu wa miundombinu ya maji kwenye vyanzo vyake hata kusababisha mmong'onyoko wa udongo kwenye mashamba ya umwagiliaji.

Inaelezwa, tembo anapopita kwenye mifereji inayopeleka maji shambani, inaharibika na kusababishia adha kwa wanaolima.

Diwani wa Kata hiyo, Boniface Mgwale, anaungana na watangulizi wake, akitaja tukio la mwanakijiji kunusurika kuuawa na baadaye baiskeli yake kuharibiwa.

"Alikuwa anatoka (eneo) Mtandika alipofika darajani pale Mlungilo akamkuta tembo ghafla, akaanza kumfukuza akafanikiwa kuingia chini ya daraja, baada ya kuingia humo, kwa hasira tembo akaanza kuiraruararua baiskeli ikawa vipande vipande, ilitenganishwa kila kitu," anasimulia.

Diwani huyo analalamika kufanyika tahmini ya uharibifu wa mazao shambani usioendana sawa na hasara anayopata mkulima, akieleza: "makadirio yao huwa hayawi sawa na hasara ambayo mkulima amepata, pia kuna ucheleweshwaji malipo kwa wakulima, hawalipwi kwa wakati na wengine hawalipwi kabisa."

Hapo Mgwale anatoa rai kwa wakazi hao wa kata, kuepuka kutembea usiku, kwa sababu mara nyingine ndio muda wa tembo kuzurura kijijini.

"Kuchelewa kurudi nyumabani hakufai. Kila mikasa ya watu kujeruhiwa na tembo inatokea usiku, kwa hiyo sipendelei sana kuona mtu anachelewa kurudi nyumbani, hata shambani nako muwe mnatoka mapema, kwa sababu huwezi kujua tembo watatokea upande gani na watakuja muda gani," anaweka angalizo la hatari.

Mwanakijiji Ziaka Kalamba, anawasilisha ushuhuda wake namna tembo, walivyoharibu vyanzo vya maji kwenye mashamba ya umwagiliaji, kwamba kila wanapopita kwenye vyanzo vya maji, basi mifereji yote huharibika.

Ni hatua inayofanya hata kijiji kiwajibike kufanye tena maendeleo ya kutengeneza mifeji ya maji, kwani vyanzo vya maji yao vinakuwa vimeharibiwa.

UCHUMI

# Maabara ya Taasisi ya Chai katika mapinduzi uzalishaji, neema shambani hadi pato la taifa

## • Kanda tatu kitaifa zavuna mamilioni ya Dola

**Na Renatha Msungu**

**DODOMA**

TAASISI ya Utafiti wa Chai nchini (TRIT), ikiwa ni chombo mama nchini katika zao hilo la kimkakati, sasa imeshakuwa kongwe katika kufanya utafiti mbalimbali wa zao hilo, ikishirikiana na wadau wa ndani na nje ya nchi.

Hapo lengo kubwa ni kuhakikisha zao chai linakuwa kiuchumi na wakati huohuo likiwanufaisha wakulima wake nchini.

Kati ya 2005 na 2006 taasisi hiyo, inaeleza kwamba ilipata aina za mbegu mpya 14 na zingine 20 zilizoboreshwa kwa kutoka Taasisi ya Utafiti wa Chai ya Kenya (TRFK), pia Taasisi ya Utafiti wa Chai ya Afrika ya Kati (TRFCA).

Mkurugenzi wa Utafiti wa taasisi hiyo ya chai, Dk. Daniel Mgori, anasema lengo lao ni kupata aina za mbegu za uhakika kukabiliana na matatizo mbalimbali kama vile ukame, magonjwa na joto lilisiloendana na mahitaji ya zao hilo, ikizingatiwa chai inahitaji baridi zaidi shambani.

Anafafanua, mbegu za kutoka nchini Kenya, mahsusi zililengwa kupata aina za mbegu zenye tija, ikiwemo kuhimili ukame na magonjwa. Hiyo ilikuwa kati ya 2005/2006 hadi 2011/2012.

Dk. Mgori anataja aina ya mbegu zenye sifa nzuri kutoka kwenye shehena zote mbili zilichaguliwa

na kuanzishiwa bustani na baadaye kutathminiwa mimea bora zaidi nchini, kulingana na mahitaji ya watumiaji na hali ya mazingira inayobadilika.

Katika hilo anasema, inafanyika kwa stadi za watafiti wanaoteuliwa, ikifanyika kazi ya kuzalisha mbegu zenye sifa nzuri kutoka kwenye mimea iliyopo na kisha kunachaguliwa mahitaji ya walaji.

Mkurugenzi huyo pia anafafanua, sasa kunafanyika utafiti ulioibua aina nane za mbegu, zilitolewa kwa wakulima nchini kati ya mwaka 2012 na 2016 na Kuthibiti Ubora wa Mbegu Tanzania (TOSCI), zikiruhusiwa kuanza kuzalishwa kitaifa.



Wataalamu wakiwa kwenye majaribio ya mbolea inayotumika kwenye zao la chai

"Tunapendekeza serikali iwekeze kwenye kusomesha wataalamu na ununuzi wa vifaa vya maabara vitakavyosaidia kuzalisha aina mpya za chai kwa njia za kisasa (Molecular Breeding and nuclear technology), ambayo inaweza kupunguza muda wa uzalishaji wa chai kwa nusu au chini ya nusu," anasema.

Kwa historia ya nchini, hadi kufika Juni 2011, zaidi ya miche milioni 62 ya chai ilizalishwa na kusambazwa kwa wakulima kwa ajili ya kujaza pamoja na kuanzishwa mashamba mapya ya chai.

Anafafanua hadi kufika Juni 2011, zaidi ya wakulima 63,900 walipata mafunzo mbalimbali ya kilimo cha chai ikiwemo uandaaji wa vitalu vya chai kwa ajili ya kuanua mashamba ya wakulima wadogo.

### MALENGO YALIYOKO

Kwa safari yake iendako, lengo mbele ni kutoa majibu kwa vitendo, yanayohusu uzalishaji chai,

kutambua manufaa yake kifedha kwa mujibu wa mapendekezo ya utafiti, kuwawasilishia wadau matokeo ya utafiti kwa njia zinazofaa na zisizo na utata.

Mengine Dk Mgori anataja, ni kueleza kuibua ufafanuzi wa visababishi vya matokeo yanayoonekana, ili matokeo hayo yaweze kutumika kwa uhakika katika maeneo mengine.

Matokeo hayo yanakaguliwa na kikundi rika kabla ya kuchapishwa kwenye maandiko ya kisayansi, katika maeneo ya: Uboreshaji wa Mazao; Usimamizi wa Matumizi Maji kwa Mazao; Usimamizi Afya na Rutuba ya Udongo; na Uhaulishaji Teknolojia.

Taasisi ya Utafiti wa Chai Tanzania (TRIT), hadi sasa inafanya kazi na wakulima katika kanda zote zinazozalisha chai nchini, ikiwemo Kanda Kuu Tatu; ikianzia Nyanda za Juu Kusini inazojumuisha Wilaya za Rungwe, Mufindi, Ludewa, Njombe na Kilolo.

Kanda ya pili inatajwa ni Milima ya Usambara inayojumuisha wilaya za Lushoto, Korogwe na Muheza na kanda ya Tatu, inayozunguka upande wa Magharibi na Mashariki mwa Ziwa Victoria, ikijumuisha wilaya za Tarime, Muleba na Bukoba.

### FAIDA YA CHAI

Hadi sasa nchini, Dk. Migori anataja Tanzania inachangia pakubwa katika kutoa fursa za ajira kwa kaya 50,000 inachangia kuendesha

maisha ya watu milioni mbili kwa ajira za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja.

Mwananchi wa Kitanzania anatajwa kuguswa kwa karibu na zao hilo, kwani nusu ya mashamba ya chai yanamilikiwa na wakulima wadogo, ambao kwa namna moja au nyingine wamepata mafunzo na mbegu bora kutoka TRIT, pindi watafiti wake wanapotoa mafunzo ya uzalishaji miche kwa wakulima

Dk. Mgori anasema, TRIT pia inajivunia kuwa sehemu ya juhudi za kuongeza uzalishaji wa chai nchini kupitia programu zake za utafiti, ugani na uhaulishaji wa teknolojia ambao umeongeza

uzalishaji kutoka tani 26,975 mwaka 2017 hadi tani 37,193 mwaka 2019.

Aidha, anasema TRIT imekuwa taasisi ya kwanza nchini kuanzisha mfumo wa umwagiliaji kwa njia ya matone (drip irrigation) kwenye chai, teknolojia ya umwagiliaji inayosaidia kutunza zao la chai kipindi cha kiangazi.

Dk. Mgori anasema ni matumizi ya teknolojia ambayo yanachangia ongezeko la uzalishaji chai

kwa kiwango cha asilimia 40, ikilinganishwa na kama mashamba yasingemwagiliwa.

### CHANGAMOTO JE?

Pia, bosi huyo ambaye pia ni mtaalamu, anasema kumekuwapo changamoto ya teknolojia hiyo kutumiwa na wakulima wadogo wanaoshindwa kumudu gharama zake.

Anasema ni uzoefu wa maabara ya TRIT kupitia ubadilishanaji wa sampuli za kimataifa, ambayo wamekuwa wakishiriki katika jaribio la mahiri wa kimataifa na ushiriki wa kimataifa linaloandaliwa na Chuo Kikuu cha Wageningen cha Uholanzi.

### MAABARA ILIVYO

Anasema, ni vipimo vinavyojumuisha udongo, mimea, samadi, mboji na majani, pia majani husika

TRIT ikilinganisha utendaji wake dhidi ya maabara nyingine zinazoshiriki kimataifa.

Dk. Migori anasifu kuwepo maabara ya TRIT, kumesaidia wakulima wa mazao mbalimbali nchini kwa kutoa majibu ya sampuli za udongo na kutoa mapendekezo juu ya nini kifanyike kwa kuzingatia matokeo ya maabara.

Tangu kuanzishwa kwake, anataja kuna sampuli 5,677 za udongo, 1,813 za majani ya mimea na 26 za mbolea, zimechanganuliwa kutoka kwa zaidi ya wateja 300 waliohudumiwa na maabara hii.

Kati ya mwaka 2015 na 2020, sekta ya chai imechangia pato la taifa kwa kuingiza Dola za Marekani kati ya milioni 28 hadi 49 kila mwaka.

Dk Mgori anasema uzalishaji mdogo wa zao la chai nchini husababishwa na mengi ikiwemo: Upatikanaji mbegu bora, matumizi madogo ya pembejeo kama mbolea na wakulima wengi kutomwagilia mashamba ya chai na jua kali.

Anataja hatua zilizochukuliwa ni ugumu wa upatikanaji mbegu bora za chai, kutolewa elimu kwa wakulima wadogo kuhusu kanuni za kilimo cha

chai na matumizi sahihi ya pembejeo na umwagiliaji wa chai wakati wa kiangazi na matumizi ya miche na mbegu bora za chai.

Inatajwa, kumechangia kuongeza uzalishaji chai nchini kutoka tani 26,975 za mwaka 2017 hadi tani 37,193 za mwaka 2019.

Dk. Mgori ana maoni kwamba kuna wakati inachukua miaka mingi, hadi kuwezesha mbegu ikaidhinishwa ikiwa na sifa kamili.

Vilevile, anaiomba serikali na wadau wengine wa maendeleo kuwekeza kwa wataalamu na vifaa vya kiteknolojia, ili kufanya uzalishaji wa mbegu bora, kupunguza hasara ya zao hilo

.



Dk. Daniel Mgori, Mkurugenzi wa Utafiti wa TRIT, akikagua shamba la chai. **PICHA: RENATHA MSUNGU.**

TAFAKURI YA MLALAHOI

# Karibuni ndugu mlioenda Kenya na somo kamili mlilojifunza huko






**NA JOSEPH KULANGWA**
Simu: +255 713 410008
barua pepe: jkulangwa@yahoo.com

NI ndoto tu! Umelala unajiona uko kwenye kituo cha kupigia kura. Unaona umati mkubwa wa watu waliojitokeza kupiga kura, lakini mambo hayaendi.

Ghafla unaona watu wanakuja na mabegi yamejaa kura, wengine wana masanduku yamejaa kura zilizopigwa tayari. Unashangaa kujiona miongoni mwa watu waliojilawa asubuhi, lakini kura zimeshapigwa!

Unachungulia ndani ya chumba cha kupiga kura huoni watu, lakini masanduku yako mezani. Kabla hujajiuliza kulikoni, ghafla sanduku lako la kura hulioni tena.

Wakati unashangaa kinachoendelea, unasikia kelele nyingi za watu wanasema hawakubaliani na hali hiyo, nawe unajikuta unapiga kelele kama hizo, ila kwa mkumbo tu. Unasogelea chumba cha kura huku ukisukuma watu mbele yako. Lakini ghafla unashitukia unadhibitiwa.

Unashituka usingizini na kujikuta kumbe uko kitandani, kumbe ni ndoto, lakini kibaya unajikuta umelimwaga kitandani. Kwa kuwa si mara yako ya kwanza kufanya hilo, unagumia tu na kujisogeza pembeni unalala tena kwa mang'amung'amu.

Wenzako uliolala nao chumbani waliokuzoea wanaunganisha doti na kujua tu tayari umeshafanya yako. Nao wanajilalia kwenye vitanda vyao usingizi wa pono.

Asubuhi wanajilawa kwenye mambo yao ya kutafuta riziki, wewe unajichelewesha ili safari hii uanike godoro kwanza. Unafanya hivyo, kisha unatoka na wewe kwenda kusaka chochote mtaani na kuhakikisha unarudi mapema ili kuanua godoro.

Unafanya hivyo na kisha unakwenda kwa jirani kupiga porojo. Huko nako kwa bahati mbaya porojo zinahusu vikojozi. Huna la kufanya, unavumilia, lakini bila kuchangia, kwani kinyozi hajinyoi.

Katika simulizi zao, unasikia wanavyoponda tabia hiyo ya ukojozi,huku wengine wakisema, ili usilimwage kitandani, ukiota unakwenda msalani usiku shituka, kwani huo ndio muda wa wewe kuharibu mambo. Kwamba ni muda ambao unajisikia mvivu kuamka na kujikuta umefanya hayo.

Unakumbuka, mbona wewe usiku ulikuwa katika matatizo ya kushuhudia watu wakicheza na uchaguzi, inakuwaje hapo kwa sababu usingeweza kushituka kwani ulitaka kutafuta haki ili kura zisichezewe kumbe ukajichezea mwenyewe?.

Kwa hiyo, ndiyo sababu watu sasa wanapigia kelele dhana ya kuwa na chombo huru kama ilivyo sauti ya majirani zetu Kenya. Hiyo ni kutokana na kuruhusiwa kuwa wagombea binafsi na mengine mengi.

Kwetu hapa mgombea asiye na chama na baadhi ya mengine, hakuna fursa hiyo, hata hivyo, tulifanya vema kupeleka watu kuwa waangalizi wa uchaguzi wa Kenya.

Walishuhudia na maana ya yaliyojiri kule ni nini. Walishuhudia mitandao ikifanya kazi wakati wote na vyombo vya habari vikitangaza matokeo bila ya kizuizi.

Hatimaye tume hiyo ya uchaguzi ikatangaza matokeo bila ya kutishiwa chochote. Wafula Chebukati hakuangalia makunyanzi, akakaa kwenye mstari wa sheria na kufanya alivyofanya.

Mliokwenda Kenya tufunzeni umuhimu wa Tume Huru ya Uchaguzi na Katiba mpya. Alamsiki!

BIASHARA

# Kijiji aina yake cha ufugaji nyuki, asali yake inarinwa kiteknolojia

**Na Elizabeth Zaya**

NYUKI ni mali na utajiri katika jamii. Ni dhana iliyo wazi, ingawaje kunahitajika kuvuka masharti ya utaalamu wake, kwa maana ya ujuzi stahiki, kuvuna yatokanayao na hitaji hilo.

Si kila mahali nyuki na asali wake wanapatikana. La hasha! Inategemea baadhi ya maeneo wanakopatikana nyuki hao, wavunaji mazao hayo wanajipanga kunufaika nayo.

Kuna baadhi ya maeneo ambako nyuki wanapatikana na kufugwa. Katika orodha hiyo, ndio panapatikana kijiji kinachojishughulisha na ufugaji nyuki maarufu Kijiji cha Nyuki kilichopo mkoani Singida.



Wafanyakazi wa Kijiji cha Nyuki, wakiendelea na kazi katika kiwanda chake cha kuchakata asali. **PICHA ZOTE: ELIZABETH ZAYA.**

Uongozi wa kijiji hicho unasema, una stadi na umahiri huo na uko tayari kutoa elimu ya kuondokana na ufugaji wa kiasili na kuhamia kufuga kibiashara.

Mkurugenzi Mtendaji wa kijiji hicho cha nyuki, Philemon Kiemi, anasema wameamua kufanya mapinduzi hayo kwa kutoa elimu katika sekta hiyo, baada ya kuzoeleka kuendeshwa kwa mazoea ya kijadi na kitamaduni kwa miaka mingi ya nyuma, bila ya kuona matunda yake.

Kiemi anasema, katika kufanikisha mapinduzi hayo kwenye sekta ya nyuki, pia wameanzisha kiwanda chenye uwezo wa kutengeneza mizinga, kuzalisha asali asilia, nta, maziwa ya nyuki, sumu ya nyuki na baadhi ya mazao kama vile gundi ya nyuki.

"Kiwanda hiki kina uwezo wa kuchakata asali tani moja kwa saa, na tunapata malighafi ya kutosha. Kwa hiyo, kijiji kimejipanga kuhakikisha kwamba katika eneo moja kunafanyika ufugaji, kuzalisha asali na kuendesha shughuli zote zinazohusina na biashara hii ili mtu anapofika anapata kila kitu," anasema Kiemi.

Anaeleza kwamba wamejipanga kuhakikisha wanazalisha mazao ya nyuki ambayo yanakidhi viwango vya ubora wa kushindana katika soko la kimataifa.

Mwenyekiti huyo anafafanua kwamba, miaka 12 iliyopita, baada ya kufahamu ufugaji wa nyuki unavyofanyika katika maeneo hayo ya Singida na mikoa mbalimbali ya nchi, wakiwatembelea baadhi ya wafugaji, ikiwemo nje ya nchi.

"Niligundua kwamba shughuli hii ni lazima iendeshwe kibiashara na si kwa mazoea na ikiwezekana, kuwepo eneo maalum ambalo mtu anaweza kuingia na kupata kila kitu kinachohusiana na nyuki," anaeleza Kiemi.

Anaendelea kwamba, pia alibaini namna wafugaji wameteseka katika upatikanaji wa mavazi yanayotumika katika shughuli hizo za ufugaji wa nyuki.

Hapo anataja mengine kama vifaa mbalimbali kwa ajili ya shughuli hizo ikiwamo mashine za kuchakata asali ambazo wameagiza kutoka nchi za Pakistan na China, ambazi zimechelewa.

**MZIZI WA KIJIJI**

Kiemi anasema kwamba, baada ya kubaini hayo, akaamua kuanzisha kijiji hicho kama kituo cha kutumika kwa shughuli zote zinazohusiana na nyuki na mazao yake.

"Changamoto hizo tulizokuwa tukipitia ndizo zilichangia kuanzishwa kwa kijiji hiki. Kwa hiyo, kwa sasa tuna eneo hili ambalo ni kubwa na ni maalum kwa shughuli zote ambalo linapatikana Itigi, Ikungi na Uyuwi,"anasema Kiemi.

Kiemi anasema, kabla ya hapo wafugaji wamekuwa wanaweka mizinga yao juu ya miti na hata baadhi yao wakapata ajali za kuanguka, ikiambatana na madhara wakati wanaendesha shughuli hizo, hali inayochangia kuleta ugumu kwa kinamama katika ufanyaji wa kazi hizo.

"Ndio maana tulisema, ni lazima tuboreshe shughuli hizi kwa sababu hakuna mtu atakayetoka mbali na kuja kutufanyia katika maeneo yetu ya asili.

"Nilipata moyo kufanya hivyo, baada ya kuona babu zangu nao walifanya shughuli hizo tangu enzi na enzi. Kwa hiyo, niliona ni rahisi kuwaelezea Watanzania mapinduzi ya shughuli hizi, kutoka kufanya kienyeji na kwenda kufanya kibiashara," anasema Kiemi.

Anaeleza matarajio yaliyoko wanategemea kuzalisha asali na mizinga mingi kufanyika katika eneo moja kwa kupitia makundi makubwa ya nyuki, kutunzwa kwenye misitu mikubwa ambayo imehifadhiwa katika mkoa wa Singida na maeneo mengine ya nchi.

Anasema kwa sasa wana jumla ya ekari 40,000 ambako kuna jumla ya mizinga 45,000 imewekwa kwenye kijiji hicho cha nyuki, sambamba na kuwepo jumla ya mizinga milioni 1.2 ya nyuki.

Pia, anafafanua zaidi: "Tumeunganisha umeme, maji, pia tumeanzisha maabara ndogo ya kuangalia usalama wa mazao yetu kwa kufuata sheria za ndani na nje ya nchi, ili kukidhi viwango vya kimataifa."

Lingine analitaja ni kijiji hicho kimechukua jukumu la kukuza utalii wa nyuki nchini, wakiwa wameanzisha makumbusho ya nyuki katika eneo hilo, lengo ni kuwasaidia watalii kujifunza ufugaji nyuki, pindi wanapotembelea eneo hilo.

"Tumegundua kwamba lipo tatizo la upungufu wa nyuki ambalo linasababisha mizinga iliyotengenezwa kutokuwa na nyuki ndani na kijiji cha nyuki kimechukua jukumu la kuandaa wataalamu ambao watashiriki katika kuzalisha makundi ya nyuki.

"Kwa sasa tuna uwezo wa kutengeneza makundi 10,000 kwa mwezi kutoka kwenye mizinga 50, 000. Tumepata 'incubators' ambazo tunachukua malikia na tunawaingiza humo, wanataga mayai na baadaye tunawalea wawe na makundi mengi na hiyo inatupa ujasiri wa kuuza mizinga na nyuki wake," anaeleza Kiemi.

Anafafanua: "Kijiji cha nyuki kimeanza kutengeneza mishumaa ambayo inatokana na nta ya asili na kwa kufanya hivyo, mishumaa itatumika katika kusherehekea siku za kuzaliwa na katika matukio mbalimbali ya mwaka mpya."

"Tunaamini kwamba kijiji cha nyuki kitakuza utamaduni wa watu ndani na nje ya nchi, kuwezesha kuuza mishumaa na tumeanzisha pia, kiwanda ambacho kinatengeneza mishumaa hii, ambayo inauzwa ndani na nje ya nchi.

"Katika kufanikisha hilo, tunawagawia pia vifaa vidogo kama vya kuchakata asali katika maeneo ya nyumbani, pia tunawafundisha maarifa jinsi ya kuandaa asali na kuepuka kuiharibu kutoka kwenye uvunaji mpaka sokoni na kwa kufanya hivyo, tutaongeza kiwango cha asali inayochakatwa kwenye kiwanda."

Mwisho anajumuisha kwa hoja kwamba, ili kuvutia zaidi watalii katika kijiji hicho cha nyuki, wameboresha zaidi mazingira kwa kuweka miradi ya michezo, sehemu za chakula ili kusaidia wanaoishi ndani ya kijiji hicho au wanaotembelea kuwa na furaha.



Bidhaa inayozalishwa katika Kijiji cha Asali, Singida.





# Bunge laridhishwa ujenzi wa makao makuu TAEC

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KAMATI ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii imeridhishwa na ujenzi wa makao makuu ya Tume ya Nguvu za Atomiki (TAEC) jijini Dodoma, huku ikitoa wito kwa Watanzania kutumia fursa hiyo kupima mionzi kwenye bidhaa zao kwa usalama wa nchi.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Stanslaus Nyongo, akizungumza jana baada ya kukagua ujenzi huo eneo la Kikombo jijini hapo, aliipongeza serikali kwa kufanikisha ujenzi huo, akisisitiza wananchi sasa wamesogezewa huduma.

"Wizara iwaeleze Watanzania watakapoanza kutoa huduma hapa ili watakaohitaji wafike hapa kwa kuwa ni makao makuu na itahudumia maeneo mengi ikiwamo ya kusini mwa Tanzania, Kigoma, Iringa, Mbeya na maeneo ya mipakani.

"Hii tume ina kazi kubwa sana ya kudhibiti mionzi na kuzuia matumizi mabaya ya mionzi kwenye chakula, simu kwa kuwa matumizi mabaya yanaweza kusababisha madhara," alisema.

Nyongo alisema kamati imeridhishwa na thamani ya fedha ambapo mkandarasi amelipwa asilimia 50 lakini ujenzi umefikia asilimia 85. Jengo hilo linagharimu Sh. bilioni 3.8.

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, alisema huduma zinazotolewa na tume hiyo zitaanza kutolewa mwaka huu kwenye makao makuu hayo.

"Wizara inasimamia utekelezaji wa juhudi za kuhamia Dodoma kulingana na vigezo na maelekezo yaliyotolewa na Ofisi ya Waziri Mkuu na sisi tunasisitiza taasisi ikihamia Dodoma isiingie gharama za kukodi pango, tunaona hapa tayari mwisho wa mwezi huu mkandarasi anasema jengo litakuwa limekamilika, hivyo tume itaingia kwenye jengo letu," alisema.

Alibainisha kuwa tume hiyo ni muhimu kwa maendeleo ya kisayansi kwenye nyuklia, usalama katika vifaa vya hospitali vinavyotumia mionzi na chakula.

Prof. Mkenda alisema serikali itaendelea kuwaendeleza wanasayansi katika masuala ya nyuklia.

Awali, Mkurugenzi Mkuu wa Tume hiyo, Prof. Lazaro Busagala, alisema ujenzi huo unahusisha maabara na ofisi za taasisi hiyo pindi itakapohamisha makao yake Dodoma.

"Kujengwa kwa ofisi hii kutaokoa gharama nyingi za uendeshaji na utawala ambazo zinasababishwa na umbali wa makao makuu ya taasisi ambayo kwa sasa yapo Arusha," alisema.

# Marufuku machinga kuwapo mtaani kuanzia Septemba 24

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KATIKA kutekeleza maagizo ya Rais Samia Suluhu Hassan ya kuwapanga wafanyabiashara wadogo maarufu machinga katika maeneo maalum, Halmashauri ya Jiji la Dodoma imesema ifikapo Septemba 24 mwaka huu, hakuna machinga atakayeendelea kubaki mtaani baada ya kukamilika ujenzi wa mradi wa soko la wazi litakalotoa huduma saa 24.

Soko hilo limegharimu Sh. bilioni 9.53 na lina uwezo wa kuchukua wafanyabiashara zaidi ya 5,000.

Mkurugenzi wa Jiji hilo, Joseph Mafuru, akizungumza na waandishi wa habari juzi ofisini kwake, alisema kukamilika kwa mradi huo ni sehemu ya utekelezaji wa maagizo ya Rais Samia aliyotoa kwa wakuu wa mikoa Septemba 13, mwaka jana la kuwapanga machinga katika maeneo maalum bila kuwasumbua katika ufanyaji wao biashara.

"Mpaka sasa tunakamilisha mradi huu ni kama mwaka mmoja umepita toka agizo hilo kutolewa. Kwanza, tunamshukuru Mheshimiwa Rais kwa kutuvumilia lakini tulitaka mradi huu ukamilike kabisa ili machinga wote tuwapatie eneo sahihi na la kudumu kwa ajili ya biashara zao," alisema Mafuru.

Alisema soko hilo lina ukubwa wa mita za mraba 14,235 na ndani yake linajumuisha huduma zote muhimu kama vile eneo maalum la kinamama kunyonyesha, kituo cha polisi, huduma za kifedha na maeneo ya vinywaji na vyakula.

"Tunataka mtu akiingia katika soko hili kila kitu akipate hapa, kama kuna bidhaa kaja kununua, basi huduma za saluni azikute hapa, akitoka arudi nyumbani siyo kwenda eneo lingine tena kutafuta huduma," alisema.

Alibainisha kuwa kati ya fedha zilizotumika, Sh. bilioni 6.5 zimetokana na mapato ya ndani kutoka katika vyanzo mbalimbali na serikali kuu iliongeza Sh. bilioni tatu. Mafuru alisema kutokana na kukamilika kwa mradi huo, machinga wote hadi ifikapo Septemba 23 mwaka huu wanapaswa kuwa wametoka mitaani.

"Hadi Septemba 24 hatutaki kumwona machinga yeyote anazunguka mitaani katika maeneo hatarishi ikiwamo kupanga bidhaa zao kwenye barabara na maeneo ya watembea kwa miguu," alionya.

Mkurugenzi huyo alisema mradi huo utaliwezesha jiji kupata mapato ya Sh. bilioni 1.2 kwa mwaka kutokana na makusanyo mbalimbali ndani ya soko.

Alibainisha faida za kukamilika kwa mradi huo kuwa ni pamoja na kuongeza hali ya usafi katika jiji kwa kuwa wafanyabiashara wadogo ndiyo wamekuwa sehemu kubwa ya uchafunzi wa mazingira. "Faida nyingine ya mradi huu ni usalama wa wafanyabiashara na bidhaa zao, lakini wanaweza kukopesheka kwa kuwa watatambulika wao na maeneo yao ya kufanyia biashara," alisisitiza Mafuru.



Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Majengo Tanzania (TBA), Daud Kondoro (katikati), akitoa maelezo kwa wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma, ilipotembelea miradi ya TBA, jijini Dodoma jana. **PICHA: RENATHA MSUNGU**

# Mil. 600/- zatumika kununua maziwa nje ya nchi kila wiki

**Na Valentine Oforo,** DODOMA

TANZANIA inalazimika kutumia Shilingi milioni 640 kwa ajili ya kununua bidhaa mbalimbali za maziwa kutoka nje ya nchi kwa kila wiki kutokana na uzalishaji mdogo na teknolojia duni nchini.

Msajili wa Bodi ya Maziwa (TDB), Dk. George Msalya, aliambia Nipashe jana kuwa Tanzania bado haina uwekezaji wa kutengeneza maziwa ya unga, hali ambayo inasababisha uagizwaji wa maziwa hayo ambayo kwa kiasi kikubwa hutumiwa na watoto wadogo.

"Kwa mfano, mpaka sasa hakuna kiwanda chochote nchini kinachojikita katika kuzalisha maziwa ya unga, hali ambayo pamoja na sababu nyingine inachangiwa na kutokuwapo teknolojia ya uzalishaji wa maziwa hayo nchini," alifafanua. Dk. Msalya alisema uwekezaji wa kiwanda cha kuchakata maziwa ya unga unahitaji mabilioni ya shilingi tofauti na kiwanda cha maziwa mengine.

"Kwa mfano, kitaalamu lita nane za maziwa ya maji hutumika kutengeneza kilo moja tu ya maziwa ya unga, mchakato ambao mbali na kuwa ghali sana, pia unahitaji upatikanaji wa maziwa mengi katika kiwanda," alisema.

Katika kutatua kero hiyo, alisema bodi hiyo ipo katika mchakato endelevu wa kuwashawishi na wawekezaji wa ndani na nje ya nchi kuja na kuwekeza katika uchakataji wa maziwa ya unga.

"Tunashukuru Mungu kwani hadi sasa jitihada zetu zimeanza kuzaa matokeo chanya, kuna baadhi ya wawekezaji kutoka wa ndani na nje ya nchi wameonyesha nia thabiti na utayari wa kuwekeza katika viwanda vya kuzalisha maziwa ya unga katika maeneo tofauti nchini," alisema.

Aliongeza kuwa Bodi ya Maziwa pia inaendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ya kuhakikisha sekta ya maziwa inakua kwa kasi na kwa viwango vinavyoakisi uhitaji wa ubora wa maziwa.

Alitaja mikakati hiyo kuwa ni pamoja na utekelezaji wa mradi wa ugawaji wa maziwa katika ofisi za wizara na taasisi mbalimbali za serikali katika Mji wa Serikali Jiji la Dodoma.

"Mpaka sasa tayari tumefanikiwa kupeleka huduma ya maziwa kwa bei ya kizalendo katika wizara 10, zoezi ambalo limeshuhudia unywaji wa zaidi ya lita 12,000 za maziwa tangu kuanzishwa kwake na kwa sasa, tunakamilisha mchakato wa kuongeza wigo wa mradi huo kwa kuongeza vituo vya kuuzia maziwa kutoka vituo 10 vilivyoko hadi vituo 20," alisema.



# Wananchi waonywa uharibifu katika mito

**Na Grace Mwakalinga,** RUNGWE

UONGOZI wa Bonde la Ziwa Nyasa umewataka wananchi wanaoishi kando ya mito yote inaoingia katika Ziwa Nyasa, kuongeza bidii katika utunzaji wa vyanzo vya maji ya mito hiyo kwa kuwa wameshika uhai wa Kamisheni ya Mto Zambezi inayoundwa na nchi nane.

Mkurugenzi wa Bonde la Ziwa Nyasa, Elice Engelbert, alitoa rai hiyo jana alipozungumza kwenye kikao cha bonde hilo kilichofanyika mjini Tukuyu wilayani Rungwe.

Engelbert alisema utafiti uliofanyika unaonyesha asilimia 59 ya maji yote ya Ziwa Nyasa yanazalishwa upande wa Tanzania, asilimia 33 ya maji hayo yanazalishwa na Malawi huku Msumbiji ikizalisha asimia nane tu ya maji yote ya Ziwa Nyasa.

Alisema Tanzania ni miongoni mwa nchi nane zinazounda Kamisheni ya Mto Zambezi na kutokana na mchango huo wa maji katika Ziwa Nyasa, inakuwa ni nchi muhimu kwa uhai wa kamisheni hiyo. "Nchi yetu ina umuhimu mkubwa katika Kamisheni ya Bonde la Mto Zambezi kutokana na mchango wetu katika uzalishaji wa maji ya Ziwa Nyasa, mchango huu unatokana na sisi Watanzania kutunza vyanzo vya maji, hivyo tunapaswa kuongeza bidii ili vyanzo hivyo viendelee kuwa salama kwa uhai wa kamisheni yetu ya Mto Zambezi," alisema Engelbert.

Baadhi ya wadau wa Bonde la Ziwa Nyasa walisema tayari wameshaanza kuchukua hatua kuhakikisha wanahifadhi vyanzo vya maji kwa kuhakikisha shughuli zote za kinadamu zinazofanyika kwenye vyanzo hivyo zinasitishwa.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe, Renatus Mchau, alisema anawatumia wataalamu wake kuhakikisha vyanzo vya maji vinalindwa, hasa kwa kuhamasisha upandaji wa miti rafiki kwenye vyanzo vya maji.

"Tumeshaanza kuwaondoa watu wote waliojenga kwenye vyanzo vya maji, lakini tunawahamasisha wananchi wetu kupanda miti rafiki kwenye vyanzo vya maji ili kuvilinda," alisema Mchau.

Mkuu wa Wilaya ya Rungwe, Dk. Vicent Anney, alitoa maelekezo kwa wataalamu wa halmashauri pamoja na wale wa Bonde la Ziwa Nyasa kuhakikisha wanalinda vyanzo vya maji kwa kutoa elimu kwa wananchi.

Alisema katika baadhi ya maeneo wameweka alama kuzunguka vyanzo vya mito mbalimbali ambako eneo kubwa la ardhi inayotumiwa na wananchi kwa shughuli za kilimo inaonekana iko ndani ya vyanzo hivyo.

Alisema katika maeneo hayo serikali haina mpango wa kuwaondoa wananchi, bali wanawahamisha kupanda mazao ya kudumu kama vile parachichi ili kutunza maeneo hayo na kulinda vyanzo vya maji.



Mkuu wa Idara ya Fiziotherapi inayojihusisha na kuwahudumia watu wenye matatizo ya uti wa mgongo, watoto wenye mguu kifundo na wenye ulemavu wa viungo katika Hospitali ya Rufani ya Kanda Mbeya, Namnyaki Abraham (kushoto), akitoa maelezo kwa viongozi wa hospitali hiyo, pamoja na wagonjwa, kuhusu utendaji kazi wa idara hiyo jana. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Makundi hatarishi tatizo uti wa mgongo yatajwa

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

ASILIMIA 70 ya wagonjwa wanaopata matibabu katika kitengo cha Fiziotherapi Hospitali ya Rufani ya Kanda Mbeya, wanasumbuliwa na matatizo ya uti wa mgongo huku chanzo kikubwa kikitajwa ni kukaa kwa muda kwenye viti ambavyo havina teknolojia ya kuepukana na tatizo hilo.

Vilevile, imebainishwa kuwa asilimia kubwa ya watu wanaosumbuliwa na tatizo hilo ni wafanyakazi wa benki, wafanyabiashara wanaouza madukani, watumishi katika taasisi mbalimbali na madereva ambao hukaa muda mrefu kwenye viti ambavyo havina teknolojia ya kukabiliana na tatizo hilo. Kwenye maadhimisho ya Siku ya Fiziotherapi juzi, Mkuu wa Idara ya Fiziotherapi Hospitali ya Rufani ya Kanda Mbeya (MZRH), Namnyaki Abrahamu, alibainisha kuwa kwa sasa watu wengi wanaofika hospitalini huko wanasumbuliwa na uti wa mgongo.

Alisema maadhimisho ya Siku ya Fiziotherapi yanatoa nafasi kwa wataalamu wa afya kutoa elimu kwa wananchi kubadili mfumo wa maisha kwa kuzingatia mazoezi na mlo sahihi ili kuzuia baadhi ya magonjwa ambayo yanaathiri mifumo ya utendaji kazi ambayo yanasababisha maumivu, athari za mjongeo na hata ulemavu.

Aliongeza kuwa taaluma ya Fiziotherapi inahusisha utendaji kazi wa mwili pamoja na mjongeo wa mwili ikiwa na lengo la kuongeza uwezo wa utendaji kazi wa viungo na mwili kwa ujumla.

Mtaalamu huyo alisema taaluma hiyo hutumia zana mbalimbali kama vile umeme, hali joto, mazoezi, elimu ya njia bora ya kuishi pamoja na uwezo wa mfiziotherapia katika matibabu kwa njia ya vitendo.

"Ni muhimu mtu mwenye magonjwa yasiyoambukizwa kumwona mfiziotherapia mapema kwa sababu moja ya kazi yetu ni kupunguza kasi ya kusambaa kwa ugonjwa, kuzuia au kupunguza usugu wa dawa, huduma yetu ambayo inaambatana na mazoezi ya viungo, umeme na hali joto, huduma zetu huleta ubora wa maisha na kurejesha mjongeo ndani ya mwili wake," alisema.

Abraham alisema wanatoa huduma ya Fiziotherapi kwa watu wenye ulemavu, wenye matatizo ya uti wa mgongo na watoto wenye mguu kifundo, lakini wanakabiliwa na uhaba wa vifaa vya kutosha kwa ajili ya kutolea huduma kama vile mashine za kunyooshea viungo.

Pia alisema hawana eneo la kutosha kwa ajili ya kutolea huduma za matibabu kwa kuwa idadi ya wagonjwa wanaohudumiwa kila siku ni takriban 100.

Alitoa rai kwa wananchi kwamba katika vita dhidi ya magonjwa yasiyoambukizwa, mfiziotherapia ndiye mtaalamu pekee aliyebobea kwenye mjongeo, shughuli za kimwili, utaalamu na ubingwa wa mazoezi tiba, pia yuko mstari wa mbele kumsaidia mgonjwa hadi anapona.

Mkurugenzi wa Hospitali hiyo, Dk. Godlove Mbwanji, aliwataka mafundi seremala kubuni teknolojia ambayo itamwezesha mtu anayeketi kwenye kiti muda mrefu kutopata madhara ya uti wa mgongo.

Alisema mafundi hao wanapaswa kuwahusisha wataalamu wa Fiziotherapi nchini ili kuwapatia ushauri wa namna gani wanaweza kutengeneza samani zitazosaidia kukabiliana na uti wa mgongo.

"Kuna watu wanauza madukani huku wameketi sehemu moja muda mrefu, kuna watumishi kama mimi ambao pia tunashinda kwenye viti, watumishi wa benki, madereva wa malori na mabasi, hawa watu wako hatarini kupata tatizo la uti wa mgongo, maana viti tunavyovitumia havina utaalamu wowote unaotusaidia kuepukana na tatizo hilo," alionya Dk. Mbwanji.

Alex Mwalyepelo, mmoja wa wagonjwa wanaopata matibabu ya Fiziotherapia katika Hospitali ya Rufani ya Kanda Mbeya, alisema huduma aliyoipata imesaidia kuleta utengamano wa mwili.

Alikumbusha kuwa mwaka 2010 alipata ajali ya gari na kusababisha majeraha kwenye viungo mbalimbali vya mwili wake, akishindwa kutembea lakini baada ya kupata matibabu katika kitengo hicho, afya yake imeimarika.

# Wataalamu wa kahawa wapata mwarobaini kuongeza uzalishaji

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WATAALAMU wa kilimo cha kahawa wameanza kuwafikia wakulima na kuwapa elimu ya kupima afya ya udongo ili kupambana na wadudu waharibifu na kuongeza uzalishaji.

Msimamizi Mkuu wa Shamba la Kahawa la Utengule Coffee, Amani Ngowi, akizungumza na Nipashe juzi, alifafanua namna walivyojipanga kuwafikia wakulima ili kupambana na ongezeko la kemikali kwenye udongo.

Ngowi alisema kuwa kwenye utafiti wao wamebaini wakulima walio wengi kushindwa kuzalisha kahawa kwa wingi kutokana na kutopima afya ya udongo, kutokujua mbolea gani inahitajika na kufanya kilimo cha mazoea na wengine kutojua jinsi ya kuzuia magonjwa ya kahawa shambani.

"Kuna magonjwa mengi yanatokea kwenye kahawa lakini wakulima wengi hawafahamu. Mfano, mwaka jana ugonjwa wa hawa wadudu wadogo ulitokea lakini wakulima hawakufahamu jinsi ya kukabiliana nao. Tunashauri wakulima wapate elimu juu ya kilimo cha kisasa, pia serikali iwasaidie wakulima wapate mbegu bora za kahawa," Ngowi alisema.

Upendo Sailosi, mkulima kutoka Utengule-Usongwe, alisema kwa sasa wanakabiliwa na tatizo la wadudu kwenye mimea ya kahawa ambao wanatoboa miti ya kahawa na kuifanya isistawi tena na hata kuoza.

Sailosi alisema siku ya mkulima ni msaada kwao kwa sababu wanakutana na wataalamu na maofisa ugani kupata elimu ya namna kukabiliana na wadudu na magonjwa mengine pamoja na kupata mbinu za kuzalisha kwa tija. Peter Mwashitete, mkulima wa kahawa, alisema mafunzo hayo yatawasaidia namna ya kuotesha mbegu za kisasa na namna ya kukata miti ya kahawa pamoja na uchumaji hadi hatua ya kuvundika.

Alisema Bodi ya Kahawa Tanzania (TCB) imewasaidia kupata mafunzo na usimamiaji mzuri zao hilo kwa kuhakikisha ubora na minada inasimamia bei elekezi iliyoko sokoni.

Meneja wa Kanda ya Mbeya wa TCB, Sijali Boa, alisema ili kufikia lengo la kuwasaidia wakulima, wameamua kuanzisha Siku ya Mkulima ili kuwasogezea karibu wakulima maofisa ugani na wadau wengine wanaohusika kwenye mnyororo wa thamani wa zao hilo na kupata mbinu za kuzalisha kwa tija.

Alisema matarajio yao baada ya mafunzo hayo ni kuona wakulima wanazalisha kwa kuzingatia kanuni za kilimo na kujikwamua kimaisha kupitia kilimo hicho.



# Serikali yaagiza upandaji miti kukabili mabadiliko tabianchi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imewataka wananchi kuotesha miti ya aina mbalimbali, ikiwamo mikoko, pembezoni mwa bahari ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi yanayoathiri maeneo wanayoishi watu na wengine kulazimika kuhama.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza, Harusi Said Suleiman, alitoa rai hiyo jana alipojibu swali la Mwakilishi wa Kojani, Hassan Hamad Omar, aliyetaka kujua mkakati wa serikali kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Alisema shida ya mabadiliko ya tabianchi imejitokeza kwa kasi katika maeneo mbalimbali, akivitaja visiwa vidogo ambapo baadhi ya wakazi wake wameanza kuhama baada ya maji ya bahari kuvamia makazi yao.

Alisema mawimbi ya bahari yanayovuma pembezoni mwa fukwe yamesababisha athari kubwa huku shughuli za kilimo zikiathirika kutokana na maji ya bahari kuingia katika mashamba ya mpunga.

"Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inazifahamu vizuri athari za mabadiliko ya tabianchi, ikiwamo maji ya bahari kuvamia maeneo ya makazi ambapo tumeshuhudia mashamba ya kilimo yakiingiliwa na maji ya bahari na wakulima kusitisha shughuli zao," alisema.

Waziri huyo aliitaja mikakati inayochukuliwa kwa sasa ni pamoja na kusambaza miche mingi ya miti aina ya mikoko ambayo ina uwezo mkubwa wa kuzuia kasi ya maji ya bahari.

Alisema serikali imeanza kujenga madaraja na kuta za kuzuia maji ya bahari kuvamia maeneo ya wananchi, maeneo ya Pemba yakijumuishwa.

Zaidi ya maeneo 150 katika visiwa vya Unguja na Pemba yanakabiliwa na tishio la athari za mabadiliko ya tabianchi.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais Zanzibar, Harusi Said Suleiman, akizungumza katika kikao cha Baraza la Wawakilishi, Chukwani, Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# ADB kusaidia ujenzi Chuo cha Ubaharia

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar imesema Benki ya Maendeleo ya Afrika (ADB) imekubali kusaidia ujenzi wa Chuo cha Ubaharia ili kuunga mkono mikakati ya serikali kuimarisha uchumi wa buluu.

Katika kikao cha Baraza la Wawakilishi jana, Naibu Waziri katika wizara hiyo, Ali Gulam Hussein, alibainisha hayo alipojibu swali la Mwakilishi wa Kojani, Hassan Hamad Omar, aliyetaka kujua ni lini serikali itaanzisha Chuo cha Ubaharia ili kwenda sambamba na mikakati yake kuingia katika uchumi wa buluu.

Naibu Waziri alisema Zanzibar imeingia katika uchumi wa buluu na suala la kuanzishwa kwa chuo kitakachoshughulikia masuala ya ubaharia ni muhimu katika kukuza uchumi huo.

Alisema ADB imekubali kusaidia ujenzi wa mradi huo kupitia mpango wa kuimarisha taaluma ya vijana katika ajira ili kukidhi soko la mahitaji ya uchumi wa buluu.

Alisema mradi huo unatarajiwa kuanza kufanya kazi katika mwaka 2023/24, akisisitiza kuwa kwa kiasi kikubwa utasaidia kutoa ajira katika sekta ya uchumi wa buluu. "Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kuwajulisha wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwamba Benki ya Maendeleo ya Afrika (ADB) imekubali kujenga Chuo cha Ubaharia kupitia mpango wa kuimarisha taaluma za vijana katika ajira kukidhi soko la mahitaji ya uchumi wa buluu," alisema. Moja ya ahadi ambazo Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amekuwa akizitilia mkazo utekelezaji wake, ni uwezeshaji wa wananchi ili kunufaika na uchumi wa buluu.

# Sababu kuchelewa taarifa watumishi waliofariki zatajwa

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais - Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora, Haroun Ali Suleiman, ametaja kilichosababisha baadhi ya wizara na taasisi za serikali kushindwa au kuchelewa kuwasilisha taarifa za watumishi wao waliofariki dunia, kuchukua likizo bila ya malipo au kufukuzwa kazi.

Katika kikao cha Baraza la Wawakilishi jana, waziri huyo alitoa ufafanuzi kuhusu suala hilo alipojibu swali la Mwakilishi wa Nafasi za Wanawake, Zainab Abdullah Salum.

Mwakilishi huyo alitaka kujua sababu zinazochangia baadhi ya wizara na taasisi za serikali kushindwa au kuchelewa kuwasilisha taarifa za watumishi wao waliofariki, kuchukua likizo bila ya malipo au kufukuzwa kazi.

Waziri Suleiman alizitaja sababu hizo kuwa ni pamoja na wakuu wa taasisi kutokuwa na utaratibu wa kupitia taarifa za watumishi walio chini yao ili kubaini hali halisi ya taarifa za watumishi hao na kukosekana kwa mfumo wa taarifa za watumishi wa kielektroniki katika ofisi kuu ya utumishi wa umma.

Alisema ofisi kuu ya utumishi wa umma tayari inakamilisha matayarisho ya mfumo wa taarifa za watumishi na mshahara utakaosaidia upatikanaji wa taarifa za watumishi katika wizara na taasisi za serikali na kuondokana na shida hiyo.

"Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais - Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora inaendelea kutoa elimu kwa watendaji na wakuu wa taasisi za umma juu ya umuhimu wa kufanya mapitio ya mara kwa mara ya taarifa za watumishi wao na kutoa taarifa ofisi kuu ya utumishi wa umma zinazohusiana na kufariki dunia, likizo bila ya malipo au kufukuzwa kazi mara tu wanapobaini kuwapo hali moja kati ya hizo kwa watumishi wao ili hatua stahiki kama vile kuwekewa vizuizi vya mshahara kuchukuliwa," alisema Haroun.

Waziri huyo alisema ofisi kuu ya utumishi wa umma itachukua hatua stahiki kwa mujibu wa sheria na kanuni za utumishi wa umma kwa wizara na taasisi zinazobainika na kuthibitika zimechelewesha au kushindwa kuwasilisha taarifa za watumishi wao zinazohitajika.

Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Saada Mkuya, alisema nia ya serikali ni kuhakikisha watumishi wake wote wakiwamo wastaafu wanaishi katika mazingira mazuri na maslahi yao yanaongezwa ili kukidhi huduma zao muhimu na kuishi katika mazingira mazuri.

"Kwa muktadha huu, wizara yangu inaangalia uwezekano wa kuboresha maslahi ya wastaafu katika pensheni kila hali itakaporuhusu," alisema.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MESHACK JAMES KAVUNGWE** anatangaza kuptea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA HARRIER** yenye usajili namba **T908 DSW , CHASSIS NAMBA: SXU 150004882** na **ENGINE NAMBA: 5S FE.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA: DSM/CEN/RB/119869/2022**

## KUPOTEA KADI YA PIKIPIKI

**DORICE FASTAEL SIAO ANATANGAZA** kupotelewa na kadi ya **PIKPIKI** yenye namba za usajili **MC 750CTM**

**Chasis Namba: MD6M14PA6L4K03291**

**Engine Namba: AK4KL4403080**

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi taarifa ya polisi RB namba

**IRI/IRI/RB/352394/2022.**

## KUPOTEA KADI YA TRAILER

**ALPHONCE GABRIEL NG'ANDE ANATANGAZA** kupotelewa na kadi ya **GARI(TRAILER)** yenye namba za usajili **T 934 ACF**

Chasis Namba: **377313**

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi taarifa ya polisi RB namba

**IRI/IRI/RB/352398/2022**

## KUPOTEA KWA VYETI



**MARIA EDWARD BUJIKU** anatangaza kupotea kwa vyeti vya taaluma ; cheti cha kidato cha nne chenye index namba S5202/0042 kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **TINGATINGA SECONDARY SCHOOL** mwaka **2015** na cheti cha kidato cha sita chenye index **NAMBA S1573/0020** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **MLANGARINI SECONDARY SCHOOL** mwaka 2018. Kwa yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA : DSM/PHQ/RB/36275/2022**

## KUPOTEA KWA KADI YA MOTOR TRICYCLE

**HARUN RASHID GUTA** anatangaza kupotelewa na kadi ya motor tricycle-**GUTA** yenye usajili namba **:MC652DJC.** kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi chochote.

**POLISI TAARIFA: ARU/ARU/RB/357598/2022**

## KUPOTEA KWA VYETI



**ELICE NATHANAELI** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S368.13** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **IMBORU SECONDARY SCHOOL** mwaka **1986.** Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA:DAR/CHU/RB/354811/2022**

## KUPOTELEWA NA HATI YA KUSAFIRIA



**DAVID MADUHU MAIGE** anatangaza kupotelewa na hati yake ya kusafiria yenye namba **TAE355610** iliyotolewa na idara ya Uhamiaji Tanzania mwaka **2020.** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa

**POLISI TAARIFA: PWA/BAG/RB/356724/2022**

**THE REGISTRATION OF DOCUMENTS ACT (CAP.117)**
**CHANGE OF NAME BY DEEDPOLL**
**BY THIS DEED.I the undersigned CASTORY HONORI SIMON of DAR ES SALAAM Tanzania, lately called CASTORI SAIMONI HONORI**



- On behalf of myself and my heirs and issue lawfully begotten absolutely renounced and abandon the use of my said name of **CASTORI SIMONI HONORI**
- For the purpose of evidencing such determination declare that I shall at all time hereafter in all records deeds and writing and in all proceedings dealing and transactions as well private as public and upon all occasions what so ever use and sign the name of **CASTORY HONORI SIMON** as my name in place of and substitution of my former name of **CASTORI SAIMOI HONORI**
- I expressly authorize and require all persons at all time to designate describe and address my heirs and issue by such adopted name of **CASTORY HONORI SIMON**

**IN WITNESS WHEREOF** I have herein subscribed my former and adopted names of **CASTORY HONORI SIMON.** This **17 day of August 2022**

**SIGNED and DELIVERED** by the said **CASTORY HONORI SIMON** formerly known as **CASTORI SAIMONI HONORI** who is introduced to me by **ISSA RAJABU** who is known to me personally this 17 day of August 2022

............................ **DEPONET.**

**(COMMISSIONER FOR OATH)**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA (MCA)**
**Mahakama ya mwanzo ya ARUSHA MJINI**
**Wilaya ya ARUSHA**
**MADAI NAMBARI 254 YA 2022**
**Mdai CHARLES LAIZER**
**amdai**
**Mdaiwa BERNARD JOSEPH SHAYO NA ELIZABETH JOSEPH**
**Kwa BERNARD JOSEPH SHAYO NA**
**ELIZABETH JOSEPH ELERAI**

**Kwa kuwa mdai /wadai ameleta/wameleta madai yake/ yao kwamba (Eleza hapa habari za madai):**

**MNAAMRIWA NA MAHAKAMA HII UFIKE BILA KUKOSA KUJIBU MADAI YA T.SHS 9,925,000/=**

**Kwa hiyo unatakiwa/mnatakiwa kuhudhuria mahakama hii siku ya ALHAMISI tarehe 15/09/2022**

Saa 02:30 asubuhi kwa kujibu madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kukatwa shauri hilo ni lazima kuleta mashahidi wako /wenu na hati zinazohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea .

Angalia kama hukuhudhuria /hamkuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu mahakama ikithibitisha kama umepokea /mmepokea kuitwa shaurini hii itaaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa /mmeshindwa .

Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 17/08/2022

.........................................
**Hakimu wa mahakama ya Mwanzo.**

## KUPOTEA KADI YA PIKIPIKI

**BARBIN JOHN MATEMU ANATANGAZA** kupotelewa na kadi ya **pikipiki** yenye namba za usajili **MC 528 CEB**

Chasis Namba: **LW8HDMZ45W003069**

Engine Namba: **WHI63ML-B4190173441**

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi taarifa ya polisi RB namba

**IRI/IRI/RB/352397/2022.**

## TANGAZO

OFISI YA KATIBU MKUU TAIFA, INAWATANGAZIA WAJUMBE WOTE WA MKUTANO MKUU WA TASO TAIFA UWEPO WA MKUTANO MKUU WA TAIFA UNAOTARAJIWA KUFANYIKA TAREHE 01.10.2022, JIJINI DODOMA TANZANIA. MUDA, UKUMBI NA KAMA KUTATOKEA MABADILIKO YA TAREHE YA MKUTANO MTAJULISHWA KWA NJIA ZA KAWAIDA NA TARATIBU ZINGINE KWA MUJIBU WA KATIBA YA TASO ZITAFUATA.TUNAWATAKIA MAHUDHURIO MEMA YA MKUTANO MKUU NA KARIBUNI SANA.

IMETOLEWA NA

.........................................
**K/KATIBU MKUU TASO TAIFA**

## FANIKIWA MICROFINANCE LIMITED
## TANGAZO LA MNADA

**Work ethic company limited** na **Kiwirilauwo investment company Ltd** Kwa idhini tuliyopewa na **FANIKIWA MICROFINANCE COMPANY** tunapenda kuutarifu umma kuwa Tutafanya mnada wa hadhara wa Nyumba Na magari katika maeneo tofauti katika jiji la Dar es salaam Na Arusha ,Wateja wanashauriwa kulipa madeni yao ndani yasiku 14 kutoka tarehe ya hili Tangazo vinginevyo Mnada utaendelea kama Tarehe za Mnada Zinavyoonekana hapa chini.

| Jina la mdaiwa | Mahali dhamana ilipo | Tarehe ya mnada |
|---|---|---|
| Asantiel Raphael Mkenda | FORD RANGERS-T204CWJ | 24.09.2022 |
| Eda Manyama Kitundu | TOYOTA HARRIER-T314 DKE | 24.09.2022 |
| JOHN NELSON MONGI | NYUMBA IPO LALASHE- ARUSHA | 24.09.2022 |
| Semen Laurent Kusundwa | Fridge | 27.09.2022 |
| Emmanuel Benjamin Komba | Printers Mbili | 27.09.2022 |
| Magesa Mngara kubebeka | Mapmbo ya nyumbani | 27.09.2022 |
| Sharifa Ally Juma | Vifaa vya salloon | 27.09.2022 |
| Paulo leonard Mwambo | Viatu vya kimasai(Sandles) | 27.09.2022 |
| Salome Sprian Nzige | Vifaa vya stationey | 27.09.2022 |

**Masharti ya Mnada.**

1. Mnunuzi atakeyeshinda atalipa 25%(au Zaidi) ya bei iliyofikwa kwenye mnada na salio la (75%)litalipwa ndani ya siku kumi nne(14) kuanzia tarehe ya mnada.
2. Endapo mnunuzi atashindwa kulipa salio kwa mda uliotolewa atakuwa amepoteza haki zote na mali itauzwa upya.
3. Ukaguzi unaruhusiwa kuanzia tarehe yaTangazo.

**Kwa mawasiliano piga 0717956315(Work ethic) au 0752605575(Kiwirilauwo) au 0677014355(Fanikiwa**


Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676









**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Russia yadaiwa kuwapeleka watoto kinguvu nchini Ukraine

**NEWYORK, Marekani**

UMOJA wa wa Mataifa umesema kwamba kuna tuhuma za kuaminika kuwa vikosi vya Russia vinawapeleka kwa nguvu watoto wa Ukraine nchini kwao.

Msaidizi wa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa kuhusu haki za binaadamu Ilze Brands Kehris. aliliambia Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa kuwa wana wasiwasi maofisa wa Russia wanautumia utaratibu uliorahisishwa wa kuwapa uraia wa Russia watoto wasio chini ya malezi wa wazazi, na kuwa watoto hao wataweza kuasiliwa na familia za Kirussia.

Alisema, vikosi vya nchi hiyo vinawaweka Waukraine katika maeneo yaliyokamatwa kupitia vituo vya ukaguzi wa usalama ambavyo vimehusishwa na matukio mengi ya ukiukaji wa haki za binaadamu.

Wizara ya Mambo ya Kigeni ya Marekani, ilisema ofisi ya Rais wa Russia, Vladmir Putin inasimamia moja kwa moja uhamishaji wa Waukraine kwenda nchini humo, na inafanya hivyo kama sehemu ya mpango wa kuyakwapua maeneo iliyoyakamata.

Lakini Balozi wa Russia, katika Umoja wa Mataifa Vasily m ameyaita madai hayo kuwa yasiyo na msingi, akisema kinachofanyika ni kusajiliwa kwa hiari nchini Russia kwa Waukraine wanaokimbia vita.

**EU kupendekeza ukomo wa bei**

Rais wa Halmashauri Kuu ya Ulaya Ursula von der Leyen, amependekeza kuwekwa ukomo kwenye bei ya gesi asilia ya Russia ili kusaidia kukabiliana kupanda kwa gharama za nishati.

Von der Leyen, ameituhumu nchi hiyo kwa kuchukua udhibiti na ushawishi wa masoko ya nishati.

Bei za nishati zimepanda kufuatia uvamizi wa Russia nchini Ukraine na kupunguzwa kwa gesi inayosafirishwa katika mabomba kwenda Ulaya.

Awali, Rais wa Russia Vladmir Putin alikosoa vikwazo vya nchi za Magharibi dhidi ya nchi yake.

Alisema Russia itachukua hatua kama nchi hizo zitaweka ukomo wa bei za gesi asilia kwa kusitisha uuzaji wa nishati kabisa.

Putin, alisema nchi yake haitasafirisha gesi yoyote, mafuta, makaa ya mawe au mafuta ya kupasha joto majumbani barani Ulaya Ujerumani yajipanga kwa nishati

Kansela wa Ujerumani Olaf Scholz, na kiongozi wa upinzani Friedrich Merz, wamekabiliana bungeni wakati wa mdahalo mkali kuhusu bajeti ya nchi hiyo.

Kupanda kwa gesi, sera ya nishati, na jinsi ya kupambana na mfumko wa bei, mada ambazo zote zinahusishwa na uvamizi wa Russia nchini Ukraine, zilitawala kwenye mdahalo huo.

Merz, aliituhumu serikali ya muungano kwa kukosa fursa rahisi za kutuliza shinikizo kwenye soko la nishati, kwa mfano kwa kudhamiria kwa uwazi zaidi kurefusha muda wa kuhudumu vinu vya mwisho vya nyuklia vinavyofanya kazi nchini Ujerumani.

Alihoji kuwa serikali pana ya muungano ya vyama vitatu inaonekana kushindwa kuchukua haraka maamuzi muhimu kwa pamoja.

Vyama vya upinzani vya siasa za mrengo wa kushoto na wa kulia vimeituhumu serikali ya Ujerumani kwa kutofanya vya kutosha kuwasaidia watu.

***DW***



Waokoaji wakifanya kazi kwenye mabaki ya treni ya ujenzi huko Hong Kong, China baada ya kuanguka juu ya makontena ambayo yalikuwa yakitumika kama ofisi za makandarasi kwenye eneo la ujenzi. **PICHA : EPA-EFE**

# Chanjo ya Malaria inatoa ulinzi kamili miaka miwili

**LONDON, Uingereza**

MAJARIBIO ya chanjo mopya ya ugonjwa wa malaria katika mataifa ya Afrika Magharibi inaonyesha kuwa inatoa ulinzi wa hadi asilimia 80 kwa miaka miwili.

Chanjo hiyo iliyotengenezwa na Chuo Kikuu cha Oxford nchini Uingereza, ilijaribiwa kwa zaidi ya watoto 400.

Maambukizi ya vimelea vya malaria yanayoenezwa na mbu, huua watoto wapatao nusu milioni kila mwaka Kusini mwa Jangwa la Sahara.

Timu ya Oxford inafanya kazi na mtengenezaji mkubwa zaidi wa chanjo duniani, Taasisi ya Serum nchini India.

Watafiti wanasema angalau dozi milioni 100 zinaweza kuzalishwa kwa gharama ya chini mwaka ujao.

Wanapanga kuwasilisha data kwa Shirika la Afya Ulimwenguni ndani ya wiki kadhaa ili kujaribu chanjo hiyo iidhinishwe.

***BBC***

## Ruto amshangaa Rais Kenyatta kutompongeza

**NAIROBI, Kenya**

RAIS mteule wa Kenya William Ruto, amelalamikia kitendo cha rais anayeondoka madarakani, Uhuru Kenyatta, kutompongeza ushindi wake.

Akizungumza na kituo cha CNN cha nchini Marekani, Ruto, alisema Kenyatta hajaona umuhimu wa kumpongeza kwa ushindi wake alioupata katika uchaguzi mkuu.

"Nimeshinda uchaguzi, hilo ndilo la muhimu, bahati mbaya Rais Kenyatta hajaona kama inafaa kunipongeza lakini nadhani ni sawa, labda amekatishwa tamaa, au hafurahi nilimshinda mgombea wake. Lakini hivyo ndivyo siasa ilivyo," aliiambia CNN.

Mahojiano hayo yalipeperushwa saa chache baada ya Ruto kuweka mtandaoni kuhusu mazungumzo yake ya simu na Rais Kenyatta, walijadili kuhusu uchaguzi mkuu na shughuli ya mpito kwa utawala mpya.

Ruto, alibainisha kwamba haki za wapenzi wa jinsia moja 'si suala kubwa nchini humo kwa sasa, na ataangazia masuala muhimu zaidi ya ukosefu wa ajira na njaa.

"Hatutaki kukuza kitu kisicho na umuhimu kukifanya kionekane kuwa na umuhimu mkubwa. Hili si suala muhimu kwa watu wa Kenya." alisisitiza

Aliongeza kuwa mapenzi ya jinsia moja na haki zao litakapokuja, watu wa Kenya watafanya uchaguzi na tutaheshimu watakachoamua, lakini kwa sasa tuangazie masuala yanayoathiri watu wetu.

Hata hivyo, sheria ya nchi hiyo inaharamisha mapenzi ya jinsia moja nchini Kenya ambayo ni adhabu ya kifungo cha hadi miaka 14 jela.

**BBC**

## Watoto 13 waokolewa wakiwa sokoni

**ABUJA, Nigeria**

POLISI katika jimbo la Rivers nchini Nigeria wamesema wamewaokoa watoto 15 kutoka nyumba moja ya mwanamke mwenye umri wa miaka 44.

Wamesema watoto hao walikuwa wametekwa nyara kwa ajili ya biashara ya usafirishaji haramu.

Watoto hao wana umri wa kuanzia miaka miaka minne hadi 15.

Walisema mwanamke huyo alijifanya kuwa mtawa. Hata hivyo, mshukiwa huyo alikamatwa na maofisa walieleza wanafanya mipango ya kuwarejesha watoto hao kwa wazazi wao.

Polisi ilisema, mvulana mmoja mwenye umri wa miaka 9 aliyeokolewa alichukuliwa kutoka sokoni Oktoba mwaka wa 2020 katika jimbo jirani la Bayelsa na tayari alikuwa ameuzwa kwa mwanamke mmoja mjini Lagos na baadae akarejeshwa Wechinwu. Usafirishaji haramu wa binaadamu ni jambo la kawaida nchini Nigeria, kwa mujibu wa shirika lisilokuwa la faida la Pathfinders Justice Initiative, huku watoto wakitekwa nyara au kulazimishwa kufanya kazi za nyumbani na biashara ya ngono.

**BBC**

# MO DEWJI AHAMISHIA MAKALI KATIKA NGUMI

**Na Saada Akida**

BAADA ya kuwa sehemu ya mafanikio katika soka la Tanzania, Mwekezaji wa Simba, Mohammed Dewji (Mo Dewji), amezindua lebo ya Mo Boxing kwa kumleta bondia kutoka Mexico, Gustavo Pina Melgar, ambaye anatarajiwa kupambana na Ibrahim Class.

Pambano kati ya Class na Melgar litakuwa chini ya lebo ya Mo Boxing Promotion na limepangwa kufanyika Septemba 30, mwaka huu kwenye Ukumbi wa Next Door uliopo jijini, Dar es Salaam.

Akizungumza jijini jana, Dewji alisema lengo kubwa la kampuni yake kuingia katika ngumi ni kudhamiria kusaidia kukuza mchezo huo hapa nchini.

Dewji, alisema anataka kuona mabondia wa Tanzania wanafanya vizuri zaidi na kuifanya Afrika kupanga ubora wa viwango.

"Dhumuni kubwa ni kukuza ndondi za Afrika kwenye jukwaa la kimataifa, kuukuza mchezo wa ndondi na kuifanya Tanzania kuwa kitovu kwa Afrika kupitia mchezo huu," alisema Dewji.

Aliongeza Mo Boxing Promotion itahakikisha inawanyanyua mabondia wenye vipaji na kutambulika kimataifa kama ambavyo wanamichezo wengine wanavyopeperusha vyema bendera ya Tanzania.

Alisema, maandalizi kuelekea pambano hilo yako katika hatua za mwisho huku akitaja pambano lingine la kimataifa litakalochezwa siku hiyo litakuwa la uzito wa mkanda wa dunia wa WBO kati ya Alfred Lamptey kutoka Ghana dhidi ya Abraham Ndauendapo.

"Tamasha hili halitavutia tu mashabiki kutoka Afrika bali litakuwa la kimataifa zaidi," Dewji alisema.

Aliwataja mabondia wengine ambao no chipukizi watakaochuana ni pamoja na Juma Choki dhidi ya Jose Hernandez, Nicholas Mwangi dhidi ya Emmanuel Mwakyembe.

Pia alisema, Sultan Al Nuaimi, atapigana na Haji Mwalugo huku Sameer Anwar akizichapa dhidi ya Mustapha Dotto na Sandra Mohammed atapambana na Lulu Kayage.

Naye mratibu wa pambano hilo, Ahmed Saddiq alisema anatarajia kutumia uzoefu wake alioupata katika Falme za Kiarabu kusaidia kuwajenga mabondia wa hapa nchini.

"Sisi (kampuni Mo Boxing), tumekuza ndondi kuanzia chini mpaka ilipo sasa kwa nchi za Falme za Kiarabu (UAE) na Kazakstan, na sasa lengo letu ni kuipandisha Afrika katika nyanja za kimataifa," alisema mratibu huyo.



Wachezaji wa Timu ya Soka ya Taifa ya Ufukweni wakifanya mazoezi kujiandaa na mashindano ya COSAFA yanayotarajiwa kufanyika kuanzia Septemba 14 hadi 20, mwaka huu katika Mji wa Durban, Afrika Kusini. **PICHA: TFF**

# Tripoli yaifuata KMKM Zanzibar

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

WAPINZANI wa KMKM katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Al Ahly Tripoli kutoka Libya ilitarajiwa kuwasili visiwani hapa jana jioni tayari kwa mchezo wa hatua ya awali ya michuano hiyo utakaochezwa kesho kuanzia saa 10:00 jioni kwenye Uwanja wa Amaan.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu wa KMKM SC, Sheha Mohammed Ali, alisema maandalizi yote yanayohitajika kuelekea mchezo huo yamekamilika.

Ali, alisema wamejiandaa vyema kuwapokea wageni wao na kuwa nao karibu katika kipindi chote watakachokuwapo Zanzibar kwa ajili ya mchezo huo muhimu.

"Kiutawala mambo yote muhimu tumeyakamilisha, tunachosubiri ni muda wa mchezo ufike, tumejipanga kucheza karata zetu vizuri, tunatarajia tutaonyesha kiwango kizuri, malengo yetu msimu huu ni kushindana na si kutolewa mapema," Ali alisema.

Naye Kocha Msaidizi wa KMKM, Ame Msimu, alisema benchi la ufundi la timu hiyo limekiandaa vizuri kikosi chake kwa ajili ya kuhakikisha wanautumia vyema uwanja wa nyumbani.

Msimu alisema wachezaji wote waliosajiliwa kushiriki mashindano hayo yanayosimamiwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF), wapo tayari kuanza vyema michuano hiyo kwa kupata ushindi.

## Ubora wanawake gofu waongezeka

**Na Shufaa Lyimo**

CHAMA cha Gofu cha Wanawake Tanzania (TLGU), kimesema mashindano ya All Africa Challenge Trophy 2022 ambayo yalifanyika kwenye viwanja vya Gymkhana jijini Dar es Salaam yalikuwa na mwitikio mkubwa.

Makamu Mwenyekiti wa TLGU, Anitha Siwale, alisema amefurahishwa na ushindani uliokuwepo katika mashindano hayo ambayo yalifanyika kwa mara ya kwanza hapa Tanzania.

"Tumefurahi kuona washiriki wanatoka katika nchi mbalimbali za Afrika, napenda niseme rasmi mashindano haya yatafungwa leo (jana) jioni," alisema Siwale.

Mwenyekiti huyo alisema hii ni mara ya kwanza Tanzania kuendesha mashindano hayo na anawaomba Watanzania waendelee kutoa ushirikiano katika kuuimarisha mchezo huo.

Alisema mashindano hayo yalishirikisha nchi 21 na kila taifa liliwakilishwa na wachezaji wanne.

## Katwila afunguka kinachoitesa Ihefu

**Na Cheji Bakari, TANGA**

BAADA ya timu yake kupoteza mechi ya tatu ya Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Zuberi Katwila, amesema wachezaji wake wamekuwa wakifanya makosa tofauti ambayo yamesababisha kupoteza michezo hiyo.

Katwila, alisema jana kila mechi imekuwa na makosa mapya, hivyo anaendelea kujipanga kuyafanyia maboresho mapungufu hayo ili wafanye vizuri katika michezo inayofuata.

"Kila mechi kunatokea makosa tofauti, makosa mengine ni ya kibinadamu na mengine ni ya kimchezo.

" Kila kosa ambalo tumelirekebisha katika mechi moja, mechi nyingine kumetokea kosa jingine, kubwa zaidi tumegundua katika mechi mbili dhidi ya Ruvu Shooting na Namungo FC ni wachezaji kukosa mawasiliano, lakini mchezo dhidi ya Mtibwa Sugar tulipotea mchezoni," alisema Katwila.

Aliongeza ili kurejesha matumaini ni lazima wachezaji wake waongeze umakini kwa sababu wakiendelea na hali hiyo itawagharimu mbele ya safari.

## ZISIKUPITE

### RASHFORD, UNITED KUTETA
KLABU ya Manchester United iko tayari kuanza mazungumzo na mshambuliaji, Marcus Rashford mwenye umri wa miaka 24, kuhusu mkataba mpya baada ya kuonyesha kiwango kizuri tangu kuanza kwa msimu huu. ***(Sun)***

### LUIZ, KEAN KUBADILISHANA
KLABU ya Juventus inataka kubadilishana wachezaji ikimtaka kiungo wa Aston Villa, Douglas Luiz na kumtoa mshambuliaji, Moise Kean mwenye umri wa miaka 22. ***(JuveLive, via HITC)***

### LUIZ: NATAKA KUONDOKA
DOUGLAS Luiz anatarajia kuondoka Aston Villa kama mchezaji huru dirisha lijalo mkataba wake utakapomalizika. ***(UOL, via Sun)***

### ICARD KUTUA GALATASARAY
KLABU ya Galatasaray imekubali kumchukua kwa mkopo wa mwaka mmoja mshambuliaji wa Paris St-German, Mauro Icardi mwenye umri wa miaka 29. ***(Fabrizio Romano)***

### MATA ANUKIA GALATASARAY
KIUNGO wa zamani wa Manchester United na Timu ya Taifa ya Hispania, Juan Mata mwenye umri wa miaka 34 pia anatarajia kujiunga Galatasaray. (Ali Naci Kucuk)

### TUCHEL AISHANGAA CHELSEA
KOCHA Thomas Tuchel ameshangazwa na kutimuliwa kwake Chelsea na aliwaomba mabosi wa klabu hiyo kumpa angalau nafasi nyingine na muda zaidi lakini waligoma**. *(Sun)***

### BARCA BADO YAJIPANGA
BARCELONA imekanusha kukataa ofa ya kununua hisa za Barca Studios iliyotolewa na mlinzi wake wa zamani, Gerard Pique mwenye umri wa miaka 35. ***(ESPN)***

### PICKFORD MAMBO MAGUMU
EVERTON haionekani kama itasajili golikipa aliye huru baada ya kuumia kwa kipa wake na wa Timu ya Taifa ya England, Jordan Pickford mwenye umri wa miaka 28. ***(Sky Sports)***

### REDMOND ANUKIA UTURUKI
WINGA wa Southampton, Nathan Redmond mwenye umri wa miaka 28 anajiandaa kufanyiwa vipimo vya afya kabla ya dirisha la usajili la Uturuki kufungwa jana Alhamisi**. *(Turkish Football, via Hampshire Live)***

### ARSENAL, EVERTON VITANI
KLABU ya Shakhtar Donetsk inataka zaidi ya pauni milioni 30 kwa ajili ya winga wake wa Ukraine, Mykhaylo Mudryk mwenye umri wa miaka 21 baada ya kusakwa na klabu za Everton na Arsenal. ***(Gianluca di Marzio, via HITC)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# KLOPP - SINA HOFU YA KUFUKUZWA LIVERPOOL

Kocha huyo asema anasubiriwa kupata ufumbuzi ingawa lolote linaweza...

**LIVERPOOL, England**

KOCHA Jurgen Klopp, amesema wamiliki wa Liverpool "wanatarajia nisuluhishe" alipoulizwa kama anaogopa kufukuzwa kama mwenzake, Thomas Tuchel.

Mjerumani mwenzake, Tuchel alifukuzwa na Chelsea Jumatano, huku mmiliki mpya wa Blues, Todd Boehly akikata uhusiano na kocha huyo wa zamani wa Paris Saint-Germain baada ya kichapo cha bao 1-0 dhidi ya Dinamo Zagreb kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Hiyo ilikuwa mechi ya 100 kwa Tuchel kuinoa Chelsea katika mashindano yote, katika miezi 18 ya usukani, aliiongoza Chelsea kutwaa ubingwa wa Ligi ya Mabingwa Ulaya, ushindi wa Kombe la Super Cup na Kombe la Klabu Bingwa Dunia.

Liverpool haijawa katika nafasi nzuri msimu huu licha ya kuibuka na ushindi wa mabao 9-0 dhidi ya Bournemouth, lakini walichapwa magoli 4-1 na Napoli kwenye mechi yao ya ufunguzi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya Jumatano.

Kilikuwa ni kipigo kigumu zaidi kupata kwa timu ya Uingereza katika mechi yao ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa tangu Arsenal ilipofungwa mabao 3-0 na Inter mwaka 2003.

Hata hivyo, alipoulizwa kama alikuwa na wasiwasi kuhusu mustakabali wake, Klopp - ambaye amekuwa Anfield tangu 2015 - aliwaambia waandishi wa habari: "Si kweli, lakini nani anajua? Tofauti (kati yetu na Chelsea) ni kwamba tuna aina tofauti za wamiliki.

"Wetu ni watulivu na wanatarajia niisuluhishe na sidhani kama mtu mwingine atafanya."

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,029,4

MECHI KALI
TANZANIA PRISONS
VERSUS
MBEYA CITY
1 | 2.39
X | 2.65
2 | 3.50

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa
vodacom m-pesa
airtel money
ZANTEL EZYPESA
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#

GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588
18+
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# XAVI: LEWANDOWSKI NI NAMBA NYINGINE



**BARCELONA, Hispania**

KOCHA wa Barcelona, Xavi amefurahishwa na mwanzo mzuri wa Robert Lewandowski katika klabu hiyo, akimtaja "hatosheki" baada ya kuwaangamiza Viktoria Plzen.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 34 alikuwa katika wakati mzuri Jumatano, akifunga hat-trick wakati Barca wakiwacharaza Plzen magoli 5-1 kwenye Uwanja wa Camp Nou.

Akicheza mechi yake ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa Ulaya akiwa na Barca, Lewandowski alifunga mabao mawili ya umbali wa yadi 20 kabla ya kufunga la tatu.

Lewandowski alikuwa mchezaji wa kwanza kufunga hat-trick katika klabu tatu tofauti kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, akiwa amefunga nne kwa Bayern Munich na moja akiwa na Borussia Dortmund.

Lakini kiwango cha Lewandowski hakikuwa cha kushangaza kutokana na kuanza kwake vizuri kwenye LaLiga na kila kitu kuhusu wiki zake za kwanza akiwa Barca.

"Robert yuko hivyo, hatosheki. Ninafurahishwa na jinsi anavyofanya mazoezi, jinsi anavyoboresha timu," alisema Xavi akiiambia Movistar.

"Ni mnyenyekevu, anatarajia (wachezaji wenzake) na anafanya kazi kubwa ya kushinikiza.

"Siyo tu hat-trick tena, ni kazi yake na jinsi anavyotawala."

# Potter kuanza na Fulham

**LONDON, England**



KOCHA wa Brighton & Hove Albion, Graham Potter amekubali kuinoa Chelsea, kwa mujibu wa 90min.

Kocha huyo mwenye umri wa miaka 47 alianza mazungumzo na Chelsea Jumatano baada ya kutimuliwa kwa Thomas Tuchel, na 90min wameambiwa mambo yalikwenda vizuri na akapewa nafasi ya kuchukua nafasi ya Mjerumani huyo huko Stamford Bridge.

Inaaminika Potter alikubali kwa mdomo kuchukua jukumu na akapeana mikono juu ya mpango huo na mkataba sasa unaandaliwa.

Chelsea wanataka dili hilo likamilishwe kabla ya leo bila matatizo yoyote, Potter atachukua usukani kabla ya mechi dhidi ya Fulham wikendi hii.

Kama ilivyothibitishwa Jumatano, mmiliki mwenza wa Chelsea, Todd Boehly alikuwa akiongoza utafutaji na kazi ilianza wiki kadhaa zilizopita wakati matatizo na Tuchel yalipoibuka mara ya kwanza.

# 401,974/-

# SPORTPESA YACHANGIA SACCOSS YA WANAWAKE WA KIZIMKAZI

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya michezo ya burudani na ubashiri Sportpesa, wikendi iliyopita imeshiriki tamasha maalum la Kizimkazi na kuchangia mfuko wa Saccoss ya kinamama kwa ajili ya kuboresha hali zao za kiuchumi.

Akizungumza wakati wa tamasha hilo, baada ya kupewa nafasi ya kutoa neno la shukrani, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Sportpesa, Tarimba Abbas, alimshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu, kwa mwaliko na pia kwa nafasi ya ushiriki. ''Napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru kwa kunialika mimi binafsi na kwa upande mwingine kampuni yetu ya Sportpesa, na pia kwa kunipa nafasi ya kutoa neno la shukrani kwa wananchi wa eneo hili".

Tarimba, alisema Sportpesa ilivutiwa na wazo la kushiriki kuchangia ama kuongeza mtaji kwenye Saccoss ya kinamama, ambapo kupitia saccoss hiyo kinamama watapata fursa ya kupata mikopo midogo midogo itakayowasaidia katika kuboresha hali zao.

"Kwa kuanzia Kampuni yetu ya Sportpesa tayari imeshatia fedha katika Saccoss hiyo ya kinamama na nisingependa kutaja kiasi ila tambueni ni fedha nyingi. Na pia inshallah mwakani pia tutaweka tena fedha zingine ili iwe chachu ya kuleta maendeleo kwa kinamama," alisema Tarimba.

Akimalizia Tarimba alimshukuru Rais Samia, kwa namna ambavyo amepeleka maendeleo katika jimbo la Kizimkazi ambapo kwa yeyote ambaye ameshabahatika kufika miaka kadhaa iliyopita ataona tofauti baina ya siku za nyuma na sasa.

"Napenda kukupa pongezi kwa namna ulivyowaletea maendeleo wananchi wa maeneo haya kwani kwa sisi ambao tumebahatika kufika hapa mara kwa mara tunaona tofauti.

Kwa mara ya kwanza SportPesa ilishiriki kwa kukarabati nyumba ya madaktari wawili ambazo zinatosheleza familia mbili ili kuhakikisha urahisi wa Wana-Kizimkazi kupata huduma pale inapohitajika.

Kama ilivyo nia ya SportPesa kuendeleza na kukuza mpira wa miguu nchini tulienda kudhamini timu ndogo ndogo za mpira wa miguu kwa kuwapatia vifaa vya michezo ikiwamo jezi.




# EATV yaandaa tamasha Oktoba

**Maulid Mmbaga na Loyce Cyriacus (SJMC)**

KITUO cha radio cha East Africa kimeingia makubaliano na The Works kwa ajili ya kuandaa tamasha maalumu la muziki litakalofanyika Oktoba Mosi, mwaka huu jijini, Dar es Salaam.

Akizungumza katika ofisi za East Africa Radio na televisheni, Mkurugenzi wa The Works, Ahmed Alli, alisema tamasha hilo litahusisha wasanii mbalimbali kutoka ndani na nje ya nchi.

Alli aliwataja baadhi ya wasanii watakaotumbuiza katika tamasha hilo ni Jay Melodi, Nyanshiski kutoka Kenya na Ruga wa Nigeria.

Aliongeza East Africa Radio na Televisheni wamesaini mkataba wa miaka miwili na The Works na lengo lake ni kushirikiana katika kuandaa matamasha ya burudani ya muziki hapa nchini.

"Kila kitu katika tamasha hili kitakuwa kikifanyika kwa mara ya kwanza, kuna mambo mengi yameandaliwa ambayo ninauhakika Watanzania watayafurahia kwa sababu ya ubunifu wa hali ya juu ulioandaliwa," alisema Alli.

Alisema kiingilio cha juu katika tamasha hilo katika eneo la VVIP ni Sh. 80,000 na VIP ni Sh. 40,000 na kuongeza tiketi zitauzwa kwa njia ya kielektroniki kupitia programu ya Nilipe.

# SUPA JACKPOT
## MECHI WIKI HII
### BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 10/09/22 | 17:00 | KV Kortrijk vs Yellow-Red KV Mechelen | 2.46 | 3.45 | 2.60 |
| 02. 10/09/22 | 17:00 | Shrewsbury Town vs Oxford United | 2.50 | 3.25 | 2.65 |
| 03. 10/09/22 | 17:00 | Birmingham City vs Swansea City | 2.80 | 3.15 | 2.46 |
| 04. 10/09/22 | 17:00 | Barnsley vs Portsmouth FC | 2.65 | 3.35 | 2.48 |
| 05. 10/09/22 | 17:00 | Southampton FC vs Brentford FC | 2.34 | 3.35 | 2.80 |
| 06. 10/09/22 | 17:00 | Leicester City vs Aston Villa | 2.45 | 3.35 | 2.70 |
| 07. 10/09/22 | 17:15 | Espanyol Barcelona vs Sevilla FC | 2.90 | 3.10 | 2.41 |
| 08. 11/09/22 | 14:30 | KVC Westerlo vs RSC Anderlecht | 2.75 | 3.35 | 2.38 |
| 09. 11/09/22 | 16:00 | West Ham United vs Newcastle United | 2.37 | 3.30 | 2.80 |
| 10. 11/09/22 | 16:00 | Sassuolo Calcio vs Udinese Calcio | 2.60 | 3.40 | 2.48 |
| 11. 11/09/22 | 16:00 | Angers SCO vs Montpellier HSC | 2.45 | 3.40 | 2.65 |
| 12. 11/09/22 | 16:00 | Leixoes SC vs SC Farense | 3.00 | 3.15 | 2.33 |
| 13. 11/09/22 | 16:30 | 1. FC Cologne vs Union Berlin | 2.48 | 3.30 | 2.65 |
| 14. 11/09/22 | 17:15 | Spal Ferrara vs Venezia FC | 2.50 | 3.20 | 2.70 |
| 15. 11/09/22 | 17:30 | FC Pacos Ferreira vs Casa Pia Lisbon | 2.70 | 3.00 | 2.65 |
| 16. 11/09/22 | 21:45 | AS Monaco vs Olympique Lyon | 2.50 | 3.40 | 2.60 |
| 17. 11/09/22 | 22:00 | Real Betis Seville vs Villarreal CF | 2.60 | 3.25 | 2.55 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### IJUMAA - 09/09/2022

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 16:00 | 3890 | Tanzania Prisons vs Mbeya City | 2.39 | 2.65 | 3.50 |
| 17:00 | 2344 | Rukh Vinnyky vs Zorya Lugansk | 3.45 | 3.55 | 1.96 |
| 17:00 | 3233 | Ararat Armenia vs Artsakh | 1.34 | 4.51 | 7.45 |
| 19:10 | 5740 | Admira Wacker vs Sturm Graz II | 2.05 | 3.48 | 3.09 |
| 19:30 | 4061 | Nurnberg vs Arminia Bielefeld | 2.18 | 3.40 | 3.05 |
| 19:30 | 5201 | Holstein Kiel vs Hamburger SV | 3.10 | 3.60 | 2.09 |
| 20:00 | 2113 | Sochi vs Dinamo Moscow | 2.08 | 3.44 | 3.24 |
| 20:00 | 2593 | Alanyaspor vs Ankaragucu | 1.74 | 3.66 | 4.42 |
| 20:00 | 2638 | Oliveirense vs Penafiel | 2.85 | 3.15 | 2.41 |
| 20:00 | 4245 | Osnabruck vs RW Essen | 2.16 | 3.45 | 3.05 |
| 20:00 | 4373 | Boluspor vs Goeztepe | 2.23 | 3.20 | 2.95 |
| 20:00 | 4763 | Sonderjyske vs Hvidovre IF | 1.92 | 3.43 | 3.48 |
| 20:30 | 1243 | FC Versailles 78 vs Dunkerque | 2.48 | 2.99 | 2.89 |
| 20:30 | 1347 | Bastia Borgo vs Concarneau | 3.74 | 3.29 | 1.95 |
| 20:30 | 2011 | Maritzburg Utd vs SuperSport Utd | 2.32 | 2.81 | 3.41 |
| 20:30 | 2510 | Saint Brieuc vs Le Puy | 2.22 | 3.08 | 3.23 |
| 20:30 | 2645 | Sedan vs Avranches | 2.64 | 3.19 | 2.54 |
| 20:30 | 2671 | Nancy vs Le Mans | 2.03 | 3.27 | 3.47 |
| 20:30 | 3199 | Villefranche Sur Saone vs FC Martigues | 2.08 | 3.24 | 3.39 |
| 20:30 | 3310 | Cholet vs Orleans | 2.75 | 3.20 | 2.45 |
| 20:30 | 4122 | Chateauroux vs Bourg Peronnas | 2.37 | 3.14 | 2.89 |
| 21:00 | 1349 | ADO Den Haag vs Jong AZ Alkmaar | 1.57 | 4.18 | 4.77 |
| 21:00 | 1427 | Almere City vs Telstar | 1.64 | 3.99 | 4.49 |
| 21:00 | 1472 | De Graafschap vs NAC Breda | 2.12 | 3.59 | 2.99 |
| 21:00 | 1539 | Jong Utrecht vs Helmond Sport | 2.18 | 3.43 | 2.99 |
| 21:00 | 2109 | FC Eindhoven vs Maastricht | 1.42 | 4.67 | 5.97 |
| 21:00 | 3676 | Roda Kerkrade vs Jong PSV | 1.54 | 4.29 | 4.99 |
| 21:00 | 4303 | FC Oss vs Jong Ajax | 3.09 | 3.74 | 2.02 |
| 21:00 | 4543 | Heracles Almelo vs VVV Venlo | 1.48 | 4.37 | 5.56 |
| 21:00 | 4642 | HNK Sibenik vs Hajduk Split | 5.89 | 4.22 | 1.44 |
| 21:00 | 5410 | PEC Zwolle vs Willem II Tilburg | 1.84 | 3.59 | 3.79 |
| 21:00 | 5571 | FC Volendam vs GO Ahead Eagles | 2.37 | 3.55 | 2.65 |
| 21:00 | 5924 | Dordrecht vs Den Bosch | 2.48 | 3.48 | 2.54 |
| 21:30 | 1320 | Dinamo Bucuresti vs CSA Steaua Bucuresti | 3.15 | 3.05 | 2.20 |
| 21:30 | 3373 | Werder Bremen vs Augsburg | 1.58 | 4.20 | 4.80 |
| 21:30 | 3715 | Palermo vs Genoa | 3.85 | 3.40 | 1.90 |
| 21:30 | 5916 | Widzew Lodz vs Cracovia | 2.65 | 3.09 | 2.50 |
| 21:45 | 1490 | Drogheda Utd vs St Patricks | 4.04 | 3.55 | 1.75 |
| 21:45 | 2748 | UCD Dublin vs Dundalk FC | 6.67 | 4.31 | 1.39 |
| 21:45 | 3217 | Tranmere vs Stockport | 2.95 | 3.15 | 2.36 |
| 21:45 | 5070 | Derry City vs Bohemians FC | 1.66 | 3.58 | 4.61 |
| 21:45 | 5165 | Waterford Utd vs Cork City | 2.41 | 3.24 | 2.65 |
| 21:45 | 5168 | St Truiden vs Standard Liege | 2.00 | 3.46 | 3.51 |
| 21:45 | 5704 | Shelbourne vs Sligo Rovers | 2.51 | 2.95 | 2.76 |
| 21:45 | 5981 | Cove Rangers vs Dundee FC | 3.39 | 3.39 | 2.02 |
| 22:00 | 1119 | Burnley vs Norwich City | 2.20 | 3.30 | 3.10 |
| 22:00 | 2017 | Lens vs Troyes | 1.47 | 4.44 | 5.85 |
| 22:00 | 3346 | Girona vs Valladolid | 2.19 | 3.18 | 3.33 |
| 22:00 | 4282 | Las Palmas UD vs Leganes | 1.91 | 3.20 | 4.10 |
| 22:15 | 5764 | Vitoria Guimaraes vs Santa Clara | 2.02 | 3.30 | 3.60 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo
Ijumaa Septemba 9, 2022
Nipashe



Klopp - Sina hofu ya kufukuzwa Liverpool



Kikosi cha Simba kikiwasili kwenye Uwanja wa Ndege jijini Lilongwe, Malawi kwa ajili ya mechi ya hatua ya awali ya mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya wenyeji Nyasa Big Bullets itakayochezwa kesho nchini humo. **PICHA: SIMBA SC**

# Mgunda afunguka Simba itapambana

## ●●●Amekiri ina kibarua kigumu Malawi huku Phiri akitamba ataendelea kupachika...

**Saada Akida na Adam Fungamwango**

WAKATI kikosi cha Simba kikiwa na wachezaji 25 kilitua salama Malawi kwa ajili ya mechi yake ya mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika, straika wake, Moses Phiri, ametamba ataendelea kupachika mabao katika kila mchezo atakaopangwa.

Simba inatarajia kukutana na wenyeji Nyasa Big Bullets katika mechi ya hatua ya awali ya michuano hiyo inayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF), itakayochezwa kesho jijini Lilongwe.

Wekundu wa Msimbazi wameondoka wakiwa chini ya Kocha Mkuu wa muda, Juma Mgunda aliyeazimwa kutoka Coastal Union akichukua mikoba ya Zoran Maki ambaye alivunja mkataba na kikosi hicho.

Akizungumza na gazeti hili muda mfupi kabla ya kuelekea Malawi, Mgunda, alisema anakibarua kigumu ambacho ni kuhakikisha timu hiyo inapata matokeo mazuri.

Mgunda alisema ana imani Simba ni timu kubwa na anaomba mashabiki kumwombea dua njema ili wafikie malengo ya kusonga mbele dhidi ya wapinzani wao, Nyasa Big Bullets.

"Kikubwa ni kuomba Mungu, nina kibarua kigumu. Simba ni timu kubwa na ina wachezaji wazuri, nitaenda kutoa ujuzi na elimu yangu kwa ajili ya kusaka matokeo mazuri katika mchezo huo," alisema Mgunda.

Aliongeza atafanya kazi kwa ushirikiano mkubwa na Kocha Msaidizi, Selemani Matola ambaye ni Mtanzania mwenzake na aliwahi kufanya naye kazi katika kikosi cha Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), kwa nyakati tofauti.

Naye Matola akizungumzia mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya KMC ambayo ilimalizika kwa sare ya mabao 2-2 alisema ilikuwa na ushindani mkubwa na wachezaji wake hawakuonyesha kiwango kizuri na kusababisha kugawana pointi.

Matola alisema makosa yamefanywa na wachezaji wote bila kujali makosa yalianzia wapi huku akikiri hawakuwa makini katika kipindi cha pili ambacho waliruhusu mabao ya kizembe.

"Ni kweli Mwenda (Israel) hakuwa na mchezo mzuri lakini hatukuweza kufanya mabadiliko kwa sababu Kapombe (Shomari) anaumwa, timu yetu leo (juzi), robo tatu hatukucheza katika kiwango chake na sasa tunaenda kujipanga kwa mchezo mwingine," alisema Matola.

Hata hivyo amewapongeza wachezaji wake kwa kupambana dakika nane za mwisho na kupata bao la kusawazisha baada ya kuwa nyuma kwa magoli 2-1.

Wakati huo huo, Phiri, ambaye amewekа rekodi ya kufunga bao kila mechi ya Ligi Kuu Bara ambayo timu yake imecheza mpaka sasa, ameahidi kuendelea kufanya hivyo kwa sababu ndiyo kazi anayoipenda.

Mzambia huyo amewatoa wasiwasi wanachama na mashabiki wa Simba kwa kuahidi watafanya vyema katika mechi ya kesho na kuwapoza machungu ya sare dhidi ya KMC. "Nimekuwa katika wakati mzuri kwa sababu nimefunga mabao matatu, moja kila mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara ambayo ni mara ya kwanza kucheza, ninawaahidi wanachama na mashabiki wa Simba nitaendelea kufunga kwa sababu ndiyo kazi yangu na ninayoipenda, ingawa kwenye mechi dhidi ya KMC nadhani wachezaji wote hatukucheza vizuri, hata mimi sikucheza vyema," alisema straika huyo wa zamani wa Zanaco ya Zambia.

Phiri alifunga bao wakati Simba ikiichapa Geita Gold mabao 3-0, alifunga goli lingine katika mechi dhidi ya Kagera Sugar iliyomalizika kwa ushindi wa 2-1 huku juzi pia akipachika bao la mapema kwenye sare ya 2-2 dhidi ya KMC.

# Azam yairejesha Yanga 'darasani'

**Na Saada Akida**

KATIKA kuhakikisha nyavu zake ziko salama, Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, amesema ameifanyia kazi maalumu safu yake ya ulinzi ili iwe imara kuelekea mechi yake ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Zalan FC kutoka Sudan.

Yanga itakuwa ugenini katika mechi hiyo ya hatua ya kwanza itakayopigwa kesho kwenye Uwanja wa Azam Complex baada ya Wasudani hao kuutumia kama uwanja wa nyumbani.

Nabi aliliambia gazeti hili amelazimika kurejea katika uwanja wa mazoezi na kuhakikisha safu yake ya ulinzi inakuwa imara baada ya mechi iliyopita mabeki kuruhusu magoli mawili.

Alisema anaamini 'darasa' jipya aliloandaa litaisaidia kurekebisha makosa ya ulinzi na hatimaye kupata matokeo mazuri katika mchezo huo wa kimataifa.

"Safu ya ulinzi ina mapungufu kadhaa naamini nimeanza kuyafanyia kazi, pia washambuliaji hawana umakini wa kutosha, yote haya tunarekebisha kabla ya kukutana na Wasudani," alisema Nabi.

Kocha huyo alisema pia anawaamini wachezaji wake wanauwezo mkubwa lakini makosa madogo madogo katika mpira hayakosekani hivyo atahakikisha anawakumbushana kuongeza umakini ili kutoyarudia.

Aliongeza Yanga haitawaona wapinzani ni timu dhaifu na badala yake watacheza kwa nidhamu na kuwapa heshima kwa sababu ni mabingwa wa nchi yao.

Yanga itarudiana na Zalan FC Septemba 17, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Zalan ni timu inayotoka mji wa Rumbek na taji lake la kwanza kutwaa ilikuwa ni mwaka 2018 ambapo ilishinda Kombe la Shirikisho la Sudan.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >